SUPA JACKPOT
TZS. 1,093,395,265
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**WAFUGAJI** watoa mapendekezo 9 Tume Haki Jinai


BUFE
Nipashe
MIAKA MIWILI YA SAMIA
Dk. Ngailo: TFRA tumeboresha kote kwa mbolea, viwanda hadi maabara
Rais azindua kilimo biashara, wadau teknolojia wabuni yao 'kumsapoti'
• Simu yaunganishwa na shughuli shambani

UKURASA 11



# Nipashe

Ijumaa Machi 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581259

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango

# Mpango: Hali ni mbaya

**AKEMEA** ushoga, ndoa jinsia moja... *Endelea ukurasa wa 2*

UKURASA WA 2

## VIONGOZI UWT WAONYWA KUWABEBA WAGOMBEA

MWENYEKITI wa Taifa wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, ameapa kuwashughulikia watendaji na viongozi watakaosababisha jumuiya hiyo kunyooshewa kidole kwa masuala mbalimbali ikiwamo kuwabeba wagombea...

UKURASA WA 3

## SHEKHE AOMBA MADANGURO YAVUNJWE KIPINDI CHA MFUNGO

SHEKHE wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, ameuomba uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Singida kuyatokomeza na kuyavunja madanguro na vijiwe vyote vya wanawake wanaojiuza mkoani hapo katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani...

UKURASA WA 4

## EACOP YACHEPUSHA NJIA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA KULINDA MAKABURI

KAMPUNI ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kwa kuheshimu mila na desturi za watu walioguswa na mradi...

## Kikwete ashinda tuzo ya usalama wa maji duniani

UKURASA 3




Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akipokea Tuzo ya Rais ya Mwaka 2023 kutoka kwa Rais wa Botswana, Mokgweetsi Masisi, iliyotolewa na Taasisi ya Global Water Changemakers, katika uzinduzi wa ripoti ya jopo la ngazi ya juu la kimataifa kuhusu uwekezaji wa maji barani Afrika kwenye Mkutano wa Maji wa Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA MAALUM**

## Polisi wahadharisha utapeli miamala fedha, laini za simu

UKURASA 2

**MICHEZO** **STARS MATUMAINI IKIWAVAA UGANDA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Mpango: Hali mbaya mmomonyoko maadili

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema hali ya mmomonyoko wa maadili, inazidi kuwa mbaya huku akikemea ndoa za jinsia moja.

Kutokana na hali hiyo, amewasisitiza wazazi kuwalea watoto wao katika maadili ya Kitanzania pamoja na kuongeza umakini katika maudhui yanayoonyeshwa kwenye televisheni.

Dk. Mpango amesema kwa sasa kumekuwapo na mmomonyoko wa maadili, ikiwamo ndoa za jinsia moja na kuwataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kukemea vikali, ili kuondokana na taifa lisilofaa kwa vizazi vya sasa na baadaye.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na waumini wa kijiji cha Kasumo mkoani Kigoma baada ya kushiriki ibada ya kawaida ya katikati ya wiki katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Malkia wa Amani lililoko kijijini hapo.

Makamu wa Rais aliwataka wazazi na walezi kuwalea watoto kwa kuzingatia maadili ya kitanzania pamoja na kuongeza umakini katika maudhui yanayooneshwa katika televisheni.

"Paroko hili ni zito, gumu kweli. Maadili ya nchi yetu yameporomoka sana. Hayo masanamu uliyokuwa ukituhubiria yamejaa, yamekuwa mengi kupindukia na mengine hata kuyasema ni ngumu.

Mimi niliyezaliwa katika kijiji hiki naogopa, ndoa za wanaume wawili, ndoa za wanawake wawili mliziona wapi? Hata wanyama hawafanyi hivyo," alisema.

"Kwa hiyo nawasihini sana, najua nyumbani kuna televisheni, mchague watoto, vijana wanaangalia nini, vinginevyo tutakuwa na taifa la ajabu kabisa," alisisitiza.

Ibada hiyo ilihudhuriwa pia na mke wake, Mama Mbonimpaye Mpango na kuongozwa na Paroko wa Parokia hiyo, Padre Joseph Mashaka.



Baadhi ya wafanyabiashara wakihamisha banda lao, ili kupisha eneo la kuegesha magari katika soko la Mbezi Mwisho mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polisi yahadharisha utapeli wa kupitia miamala, laini za simu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limewatahadharisha wananchi kuhusu utapeli mpya unaofanywa na baadhi ya vijana wanaojitambulisha kama mawakala wa kampuni za simu na kuiba fedha kwenye akaunti zao.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), David Misime, aliyasema hayo juzi wakati wakizungumza na wananchi wa Kata za Kibondemaji A na Mbagala Kuu kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Zakhiem, Mbagala mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuna utapeli unaojitokeza sasa hivi wa baadhi ya vijana wanaopita mitaani wakijitambulisha kuwa mawakala wa kampuni za simu na kuwarubuni wananchi na kuwaibia fedha kwenye akaunti zao za simu au benki.

"Vijana wanaotekeleza uhalifu huu utawatambua kwa maneno yao ambayo ni tofauti na mawakala wa kweli kutoka katika kampuni za simu.

"Mawakala halali wa kampuni za simu hawapewi maelekezo ya kumwambia mteja mara atoe laini yake ya simu ili aiweke kwenye simu yake kwa ajili ya kukuhudumia," alisisitiza. Pia aliwaambia wananchi hao kuwa wakiona watu wanaowaambia hivyo, wakatae kuwa huo ni tapeli, hivyo watoe taarifa polisi. "Ukiona anakwambia nunua muda wa maongezi au hamisha fedha kutoka akaunti yako ya simu huyo ni tapeli," alibainisha.

Misime aliwataka wananchi wasikubali kupewa huduma holela za mitandao ya simu au za kifedha mitaani na badala yake wafike kwenye ofisi zilizosajiliwa kihalali. Pia aliwaeleza kuwa wasikubali kutoa namba zao za siri au kutoa laini kuwekwa kwenye simu za matapeli hao wanaojiita watoa huduma mitaani.

Akizungumzia kuhusu kundi la vijana maarufu kama 'Panya Road' linalofanya vitendo vya uhalifu, Kamishna Msaidizi Mwandamizi mstaafu, Engelbert Kiondo, alisema wanaojihusisha na vitendo hivyo ni zao la mmomonyoko wa maadili unaochangiwa na wazazi kuwa na mapenzi na watoto badala ya kuwapa malezi bora.

Alisema jamii inaweza kumaliza tatizo hilo kama wananchi wataridhia kushirikiana kwa karibu na polisi kata katika maeneo yao.

Mrakibu wa Polisi kutoka Kamisheni ya Polisi Jamii, Makao Makuu ya Polisi, Dk. Ezekiel Kyogo, aliwataka wananchi wa Mbagala kuwa wazalendo na nchi yao.

Alisema kwa kufanya hivyo watakuwa na uthubutu wa kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu na kufichua wahalifu.

Dk. Kyogo alisema Jeshi la Polisi kwa sasa moja ya mikakati yake mikubwa ni kuhakikisha linashirikisha wananchi katika kubaini na kuzuia uhalifu kuliko kupambana baada ya kutokea.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
23/03/2023

TAARIFA KWA UMMA

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **24/03/2023** Kampuni ya **TRANSCONNECT LOGISTICS T LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Tunduma kupitia Mikumi.

Gari yenye namba zifuatazo:
**T363DEY / T509AZD**

VIPIMO

**Urefu – 17.40m** **Upana – 5.10m,** **Kimo 4.65m**

Gari litasafirisha mzigo kuanzia saa12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


# Viongozi UWT waonywa kuwabeba wagombea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Taifa wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, ameapa kuwashughulikia watendaji na viongozi watakaosababisha jumuiya hiyo kunyooshewa kidole kwa masuala mbalimbali ikiwamo kuwabeba wagombea.

Aidha, amesema hatosita kuchukua hatua za kinidhamu kwa yeyote atakayethibitika kuendeleza makundi, awe mbunge, mwakilishi au kiongozi wa UWT.

Akifunga juzi mafunzo ya viongozi wa UWT ngazi mbalimbali jijini hapo, Chatanda, alisema ni vyema watu wanaotamani kuwa wabunge na madiwani wakapunguza hamu ili kuwaacha waliopo madarakani wakamilishe muda wao. "Tusubiri muda utakapowadia kila mtu ataingia uwanjani kwa watendaji na viongozi watakaobeba wagombea kabla ya wakati hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao, pia tuachane na kuchukizwa na rushwa sisi tupaze sauti kwa kukemea na kuonesha mfano."

"Haya ninayoyasema hapa ya kuanza kampeni kwenda kujipitisha pitisha kabla yanasababisha kutoa rushwa, hawezi kuja mkono mtupu na wewe unasema mimi ndio mwenyewe hapa, ni marufuku tuwaache wabunge wafanye kazi zao na madiwani muda ukitimia mtaingia," alisema.

Alisema hakuna faida yoyote ya kuwa na fitina na uchonganishi kwa kuwa hayaleti afya kwa UWT.

"Achana na fitina ndogo ndogo katika uongozi wangu nataka kuongoza UWT yenye umoja, tunapaswa kuwapa ushirikiano viongozi wanaotuwakilisha kwenye vyombo vya dola, wabunge na madiwani badala ya kuanza sasa kupanga safu, kujipitisha kabla ya muda, tupunguze hamu ili tuwatendee haki waliopo madarakani," alisema.

Alisema watakaojipitisha kwenye majimbo na kata watasababisha wabunge kukosa utulivu bungeni na kwenda kukimbizana.

"Nimeanza kupata taarifa na malalamiko kwa baadhi ya wabunge watu wameanza kujipitisha huko, huko kujipitisha kukome kuanzia leo, tumeweka utaratibu ufuatwe. Tukikubamba ndugu zangu andika umeumia wewe usichukue fomu 2025," alisema.

Kadhalika, alikemea makundi na kwa sasa Mwenyekiti na Makamu wake hawana kundi, UWT ni moja na yeyote mwenye maono anakaribishwa ili kujenga.

"Msiendeleze makundi kwenye mikoa na wilaya kwa wabunge na madiwani wa viti maalum wahakikishe makundi ya uchaguzi yanavunjwa, katika uongozi wangu nataka kuongoza UWT yenye umoja, mshikamano na upendo isiyo na makundi, sitakubali jumuiya inyooshewe kidole hasa wakati huu ambao tuna Mwenyekiti wa CCM mwanamke na Rais," alisema.

Aliwataka kujipanga namna ya kuwapata viongozi wa serikali za mitaa kwenye uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwaka 2024.

HABARI KITAIFA

# Kikwete ashinda tuzo ya usalama wa maji duniani

**Na Jenifer Gilla**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete ameshinda tuzo ya heshima ya kimataifa inayotolewa kwa viongozi wa juu wanaoleta mabadiliko duniani katika sekta ya maji (Global Water Changemakers Award) kwa kuonyesha dhamira ya juu ya kisiasa na uongozi katika kufanikisha usalama wa maji unaostahimili mabadiliko ya hali ya hewa barani Afrika.

Alikabidhiwa tuzo hiyo na Rais wa Botswana na Mwenyekiti wa tuzo hiyo, Mokgweetsi Masisi, juzi, wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Jopo la Ngazi ya Juu la Kimataifa kuhusu Uwekezaji wa Maji Barani Afrika katika Mkutano wa Maji wa Umoja wa Mataifa uliofanyika, New York, nchini Marekani.

Pia, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepata tuzo hiyo kwa ngazi ya kitaifa baada ya uzinduzi wa mpango wa uwekezaji wa maji, visiwani humo.

Viongozi wengine waliopata tuzo hiyo kwa ngazi ya kimataifa ni Rais wa Senegal na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Macky Sall, Rais wa Namibia, Hage Geingob na Waziri Mkuu wa Uholanzi, Mark Rutte huku Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, akipata tuzo kama hiyo kwa ngazi ya kitaifa kufuatia uzinduzi wa Mpango wa Uwekezaji wa Maji katika nchi hiyo.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji wa tuzo hiyo ilieleza kuwa madhumuni ya Jopo la Ngazi ya Juu la Kimataifa la uwekezaji wa maji barani Afrika ni kuendeleza njia zinazoweza kutekelezeka za kukusanya Dola bilioni 30 (Sh. trilioni 70) kila mwaka ifikapo 2030, kwa ajili ya kutekeleza programu hiyo ili kuziba pengo lililopo la uwekezaji wa maji barani Afrika linalokadiriwa kuwa Sh. trilioni 45.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo zaidi ya Waafrika milioni 300 hawana huduma majisafi ya kunywa na zaidi ya milioni 700 wanaishi bila huduma bora za vyoo.

Aidha, takriban Dola za Marekani bilioni 50 (Sh. trilioni 117) kila mwaka sawa na Dola za Marekani 40 (Sh. 94,000) kwa kila Mwafrika zinahitajika, ili kufikia usalama wa maji na usafi wa mazingira endelevu ifikapo mwaka 2030.

Tuzo ya Waleta Mabadiliko ya Maji 2023 hutolewa kwa viongozi wa juu ikiwamo marais kutambua mchango wao wa kujitolea kwa hali ya juu katika uwekezaji wa sekta ya maji unaoyostahimili mabadiliko ya hali ya hewa, ili kusaidia usalama wa maji duniani ambao hutunukiwa katika hafla ya kimataifa ya Umoja wa Mataifa (UN).



Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wa Jiji la Dodoma, wakiandamana kwa ajili ya kupongeza mafanikio ya miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Shekhe aomba madanguro yavunjwe kipindi cha mfungo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHEKHE wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, ameuomba uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Singida kuyatokomeza na kuyavunja madanguro na vijiwe vyote vya wanawake wanaojiuza mkoani hapo katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Shekhe Nassoro alitoa ombi hilo jana wakati akifunga mafunzo ya wahitimu wa dini ya kiislam katika Madrasa ya Siraj iliyopo msikiti wa Kibaoni, Manispaa ya Singida.

"Kwa heshima hii ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani naiomba Serikali ya Mkoa wa Singida, kuhakikisha madanguro yote yaliyopo mkoani Singida yanatokomezwa, madiwani kupitia kata zao kwa kushirikiana na mashekhe na wajumbe wa mabaraza wasaidie kutokomeza madanguro hayo," alisema.

Alisema haipendezi kuona kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani madanguro yanaendelea kuwapo mitaani na kufanya mambo ambayo hayampendezi Mwenyezi Mungu.

Katika hatua nyingine aliwataka waumini wa dini ya Kiislam mkoani hapo kuacha tabia ya kuwabeza, kuwadhalilisha na kuwashutumu walimu wa dini badala yake watambue thamani yao.

Alisema Waislam wanatakiwa kutambua kuwa walimu hao sio malaika bali ni wanadamu wana upungufu kama ilivyo kwa watu wote na wachukue yaliyo mema kutokana na hadhi yao.

Alisema walimu hao wa dini wanafanya kazi kubwa katika madrasa mbalimbali katika hali duni, hawana posho huku mishahara yao ikiwa ni matusi, kudhalilishwa na kupewa maisha mabaya.

Aliwaomba Waislam kuanzia sasa kujenga utamaduni katika misikiti kuhakikisha linapatikana fungu la walimu hao wa madrasa.

Aidha, aliwataka walimu wa dini kusimamia maadili kwa watoto wa kiislamu hasa katika kipindi hiki cha sasa ambacho dunia inawaangaza watoto wa kiume katika kuleta hadaa ya kuwaghilibu ili wawe mabaradhuli, mashoga. "Sitopendezewa, sitofurahi, sitosikia amani kusikia moja ya madrasa kuna watoto ambao wameanza kuwa mabaradhuli," alisema.

Aliwaasa katika kata zao kuwasemea Waislam na kuupigania uislam.

Alisema hivi sasa wanaingia katika kipindi cha mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani moja ya wajibu wao ni kujua idadi ya Waislam waliopo kwenye maeneo yao hasa watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo yatima jambo litakalosaidia kuwapatia misaada ya kibinadamu.

Alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwaonya wafanyabiashara wasipandishe bei ya vyakula katika mwezi huu kama alivyofanya Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

# Wafugaji watoa mapendekezo 9 Tume ya Hakijinai

**Na Restuta James**

WAFUGAJI wamewasilisha mapendekezo tisa kwenye Tume ya Rais ya Kurekebisha Mfumo wa Hakijinai, wakitaka serikali itenge maeneo ya malisho na iache kutaifisha mifugo inayoingia kwenye Hifadhi za Taifa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Mrida Mshota, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya kuwasilisha maoni yao mbele ya tume hiyo inayoongozwa na Jaji mstaafu, Othman Chande.

Alisema kutengwa kwa maeneo ya malisho kutaepusha migogoro kati ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi.

Alisema pendekezo hilo linalenga kuwapa wafugaji maeneo yanayokidhi mahitaji yao, kama inavyofanyika kwa wakulima, mapori ya akiba na tengefu; Hifadhi za Taifa na Misitu, akilalamikia kwamba wafugaji wamekuwa wakihamishwa kutoka eneo moja kwenda lingine bila kujali kama lina mahitaji muhimu ambayo ni malisho au maji.

Kadhalika, wametaka maboresho ya sheria tisa wakitaka wakuu wa wilaya wanyang'anywe mamlaka ya kukamata na kuweka watu ndani.

Katika hilo, wametaka Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kifungu cha 177 (3) kifutwe. Kadhalika, wamependekeza Sheria ya Uhujumu Uchumi sura namba 200 kifungu cha 36 (2) na (3) kirekebishwe ili makosa yote yawe na dhamana na Mwendesha Mashtaka (DPP), asiruhusiwe kuzuia dhamana kwa mtuhumiwa yeyote.

Wafugaji wamependekeza pia marekebisho ya Sheria ya Wanyamapori sura ya 283 vifungu vya 18 (4) na 21 (2), kuhusu kukamatwa kwa mifugo inayoingia hifadhini na kwenye mapori tengefu, mapori ya akiba na faini zinazotozwa wakieleza kuwa adhabu ni kubwa.

Alisema sheria hiyo inataka mmiliki wa mifugo aadhibiwe inapoingia kwenye hifadhi na badala yake, inatumika kutoza faini kwa kila ng'ombe, mbuzi au kondoo, anayekutwa kwenye maeneo hayo.

Mwanasheria wa CCWT, Denis Shangai, alitaja sheria nyingine kuwa ni Sheria ya Jeshi la Polisi sura 322 kifungu cha 47 kinachotaka liwekwe tangazo gazetini kwa miezi sita ili mwenye mali hiyo ajitokeze, lakini kinatumiwa vibaya na vyombo vya dola kutaifisha mifugo inayoingia kwenye hifadhi.

Alisema Ibara ya 24 ya Katiba ya mwaka 1977 inazungumzia haki ya kumiliki mali kama moja ya haki za binadamu na kwamba haki hiyo inanyang'anywa na vyombo vya dola vinavyotaifisha mifugo.

"Ukamataji, utaifishaji na uuzaji wa mifugo ni kinyume cha Ibara hii ya Katiba," alisema.

Shangai alitaja sheria nyingine inayowaumiza wafugaji ni ya Hifadhi za Taifa sura ya 282 kifungu 25 (1)(d) na kanuni zake ambazo alidai kinatumiwa vibaya kutaifisha mifugo. Kwa mujibu wa Shangai, sheria nyingine wanayopendekeza irekebishwe ni ya msaada na huduma ya Polisi sura ya 322 (47) (7) na Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2012.



Meneja Mkuu wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) Tanzania, Wendy Brown (kulia), akishuhudia zoezi la utiaji saini na jamii ya Wataturu, ili kuruhusu uchepushwaji wa bomba la mafuta ghafi katika makaburi yao ya kimila katika kijiji cha Mwamayoka, wilayani Igunga, mkoani Tabora mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EACOP yachepusha njia mradi wa bomba la mafuta kulinda makaburi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kwa kuheshimu mila na desturi za watu walioguswa na mradi, imetia saini mkataba wa kusimamia haki na kuheshimu utamaduni wa wazawa na jamii ya Wataturu wanaoishi katika Kijiji cha Mwamayoka, Igunga mkoani Tabora kwa ajili ya kuchepusha njia ili kuyalinda makaburi yao ya kimila.

Awali, watu wa jamii hiyo walikuwa na wasiwasi wa kuathiriwa kwa makaburi yao yaliyoko eneo la Bung'enda na maeneo yao mengine kadhaa ya kuabudia endapo mradi ungeanza ujenzi.

Akizungumza wakati wa kutia saini makubaliano hayo juzi, Mkurugenzi Mkuu wa EACOP Tanzania, Wendy Brown, alisema baada ya majadiliano na jamii na viongozi wa kimila, kampuni ilifanya mapitio ya kiufundi na kukubali kupitisha bomba hilo katika njia mpya ili kutokuwa na athari yoyote katika maeneo muhimu ya kimila na kiutamaduni.

Alisema EACOP inaheshimu haki na mila za makundi yote ya kikabila yanayoguswa na mradi, hivyo itaendelea kushirikiana na jamii zote zilizoguswa na mradi pamoja na viongozi wao wa kimila ili kuhakikisha maoni yao yamezingatiwa wakati wote wa kupanga na kutekeleza mradi.

Mkataba huo ni wa pili kutiwa saini na EACOP baada ya ule wa kwanza na jamii ya Akie inayoishi Kanda ya Kaskazini.

Alisema kutiwa saini kwa mikataba hiyo ni kielelezo tosha kuwa mradi wa EACOP unashirikisha makundi yanayoguswa katika ngazi zote za utekelezaji na kuheshimu mila, utamaduni na haki za jamii husika.

Brown aliongeza kuwa mradi wa EACOP unatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, jamii na utunzaji wa mazingira.

Gesuda Masanja, ni chifu wa jamii ya Wataturu alipongeza hatua ya EACOP kwa kuzingatia mila zao na kusema mradi huo utasaidia kwa maendeleo ya jamii ya kabila hilo.

Awali, Martha Bayo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, alipongeza hatua ya EACOP na kuitaka jamii ya Wataturu kuwa walinzi wa bomba hilo la mafuta ghafi litakapokamilika.

Naye Lucas Bugota, Diwani wa Kata ya Igunga, aliusifu mradi wa EACOP kwa hatua hiyo, alisema jamii ya Wataturu imeweka historia katika kulinda mila na tamaduni zao.

Nailejileji Tipap kutoka Jukwaa la Wafugaji lisilokuwa la Kiserikali (Pingos Forum) alisema hatua ya kampuni ya EACOP kutia saini mkataba huo inalinda maslahi ya jamii ya Wataturu hao.

# Ofisa TRA atoa ushahidi kesi ya udanganyifu

**Na Kulwa Mzee**

OFISA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Edith Ignas (57), amedai polisi walimtaka atoe taarifa za umiliki wa magari sita yanayobishaniwa katika kesi ya udanganyifu inayomkabili Shabani Cosla na dalali wa mahakama.

Ignas ambaye ni shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka, alidai hayo katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Susan Kihawa.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Kija Elias, shahidi huyo aliyekuwa kitengo cha kusimamia usajili wa magari na leseni, alidai Oktoba 5, 2021 akiwa kazini alipokea barua kutoka polisi ikimtaka atoe taarifa za umiliki wa magari.

Alidai kuwa alitakiwa atoe historia ya umiliki na anwani za wamiliki, hivyo barua ilihitaji taarifa za magari sita na alifanya hivyo na ku-print (toa nakala) kila taarifa ya gari akaambatanisha na barua ya polisi.

Shahidi alidai kuwa kila gari lilikuwa na mmiliki wa kwanza na taarifa ilionyesha hadi mmiliki wa mwisho.

"Nilijibu barua ya polisi, wamiliki wa magari hatuwajui kwa sura,"alidai shahidi.

Shahidi wa pili, Henglibet Barnabas kutoka Wakala wa Usajili wa Leseni na majina ya Biashara (BRELA), alidai kuwa alipokea barua ya polisi ikitaka taarifa za kampuni sita.

Anadai walitaka taarifa za Kampuni ya Escon Borewell, Excon Borewell, Target Borewells, SBJ, Simba na Fahak.

Shahidi alidai alipoangalia alikuta Kampuni ya Escon ilikuwa haina usajili, iliyosajiliwa ni kampuni ya Excon ambayo ilibadili jina na kuitwa Simba.

Alidai kampuni zingine tatu zilikuwa zimesajiliwa na zinaendelea kufanya kazi na tangu zisajiliwe hazijawahi kubadili majina.

Katika shauri hilo washtakiwa wanadaiwa kutoa taarifa za uongo mahakamani, kuhamisha umiliki wa magari 14 na kujipatia fedha kwa udanganyifu.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 31 yakiwamo ya kutoa taarifa za uongo 27, kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu matatu na moja la kujipatia fedha kwa ulaghai.

Mshtakiwa wa pili, dalali wa mahakama, Charles Sengo, miongoni mwa mashtaka yake ni kuonyesha magari yaliuzwa katika mnada wa hadhara wakati si kweli.

Pia mshtakiwa wa kwanza miongoni mwa mashtaka yanayomkabili, anadaiwa Aprili 11, 2019 akiwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Fahak, kwa ulaghai alijipatia Sh. milioni 185 kutoka katika akaunti ya mahakama iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BoT) namba 99212697226 kwenda kwenye akaunti ya kampuni yake namba 0150515062000 akionyesha fedha hizo zilipatikana katika mnada uliofanyika Septemba 11, 2016 wakati si kweli.

# Wananchi waondolewa hofu upatikanaji chakula

**Na Pendo Thomas,** MWANZA

WANANCHI wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wameondolewa hofu na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) Kanda ya Ziwa kuhusu upatikanaji wa chakula pamoja na mfumuko wa bei hususani katika kipindi hiki ambacho mikoa hiyo imeathirika na ukame baada ya serikali kuongeza uzalishaji kupitia viwanda vinavyomilikiwa na bodi hiyo.

Akizungumza kuhusu upatikanaji wa nafaka kwenye mikoa hiyo juzi Kaimu Meneja wa CPB Kanda ya Ziwa, Alfred Kalimenze, alisema kwa sasa serikali imejipanga kukabiliana na mfumuko huo kupitia viwanda vyake ili kusaidia upatikanaji wa chakula hususani mchele kwa bei ya chini ikilinganishwa na iliyopo kwenye masoko ya nafaka nchini.

Kalimenze alisema wanatarajia kuongeza kiwango cha ukusanyaji mazao hasa mpunga kutoka tani 5,000 hadi 20,000 ongezeko linalotarajiwa kukuza usambazaji wa mchele wenye bei nafuu kwenye masoko ndani ya nchi na nchi za Afrika Mashariki ambazo zinanunua mchele nchini.

Aliwataka wananchi kuendelea kutumia fursa ya vituo vilivyo katika maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo ili kupata nafaka kwa bei nafuu kama hatua ya kuwapa unafuu wananchi.

Ofisa Masoko na Mauzo wa bodi hiyo, Ally Mango, alisema hadi sasa katika kiwanda kikubwa cha kuchakata zao la mpunga wamechakata tani 5,594 na kufanikiwa kupata mchele tani 3,394 ambazo ziliuzwa ndani na nje ya nchi.

Katika uzalishaji huo, Mango alisema tani 700 za mchele zimeuzwa nchini Uganda, 600 (Rwanda) na 400 (Kenya) na jumla ya mauzo ya ndani na nje ya nchi walitengeneza faida ya Sh. bilioni 1.8.

"Asilimia 60 ya mauzo yetu tumeuza nchi jirani sisi ndio wazalishaji wakubwa wa zao la mpunga Afrika Mashariki, tunafurahia fursa hii ya kufanya biashara ya mchele ikilinganishwa na nchi zinazotuzunguka," alisema Mango.

Naye msimamizi wa kiwanda hicho, Mhandisi Nasra Majio, alisema uzalishaji wao unakubalika kwa vigezo vya ndani na nje ya nchi kutokana na kuwa na mashine za kisasa zinazotumika kuchakata nafaka kwa ubora.

Kiwanda cha usindikaji wa mchele kinachomilikiwa na Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko kina uwezo wa kukoboa zaidi ya tani 90 na kuwa fursa kwa wakulima wa mpunga kuuza kwa bei rafiki tofauti na ya walanguzi.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Tanzania, Omary Itambu (kushoto), akisoma kitabu chenye ujumbe wa lishe kwa watu wasioona, ikiwa ni ishara ya kundi hilo kufikiwa na elimu ya masuala ya chakula na lishe, kilichoandaliwa na Taasisi ya Chakula na Lishe kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe, Dk. Ray Masumo. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Kesi daktari anayedaiwa kunajisi yakwama

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kunajisi na kulawiti binti wa miaka 21 inayomkabili daktari wa Hospitali ya Rufani ya Amana, Joseph Mwaipola (50), imeshindwa kusikilizwa mahakamani kwa sababu wakili wa serikali anayeendesha kesi hiyo kutokuwapo.

Taarifa iliwasilishwa jana na Wakili wa Serikali, Monica Ndakidemi, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa.

Ndakidemi aliiomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine ya kusikilizwa kwa sababu wakili anayeendesha kesi hiyo ana majukumu mengine.

Hakimu Ruboroga aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 28, 2023 kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Ilidaiwa kuwa katika shtaka la kwanza, Mwaipola ambaye ni Mkazi wa Mtoni Kijichi anatuhumiwa katika tarehe zisizofahamika kati Februari, 2022 akiwa eneo la Hospitali ya Rufani ya Amana, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam alimnajisi binti wa miaka 17.

Katika shtaka la pili, anadaiwa Mei 31, 2022 akiwa katika nyumba ya kulala wageni ya Panzuri iliyopo Temeke, ndani ya Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam alimbaka binti wa miaka 17.

Imedaiwa kuwa, kati ya Februari, 2022 mshtakiwa akiwa eneo la Hospitali ya Amana, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam alimlawiti binti mwenye miaka 17.

Mshtakiwa alikana kuhusika na tuhuma hizo na kudhaminiwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho na kitambulisho cha Taifa au cha kupigia kura.

Pia wadhamini hao pamoja na mshtakiwa walisaini bondi ya Shilingi milioni tano kila mmoja.

# Uhamishaji makaburi kupisha reli waendelea

**Na Frank Monyo**

UHAMISHAJI makaburi kwa ajili ya kutwaa ardhi itakayojengwa Reli ya Kisasa - SGR mkoani Tabora, kipande cha tatu, Makutupora - Tabora unaelekea kukamilika.

Makaburi hayo yako katika halmashauri za Tabora, Itigi, Manyoni na Sikonge. Ujenzi wa SGR katika kipande hicho umefikia takribani asilimia 5.52.

Akizungumza wakati wa kikao cha viongozi na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Manyoni, Mrakibu (SP) Ahmed Makele, alilishukuru Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa kuanza uelimishaji kwa wananchi na viongozi kuhusu utwaaji ardhi na kutoa wito kwa serikali ya kijiji na ndugu wa marehemu kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha mchakato huo unakwenda salama. "TRC mmefanya jambo la msingi sana kuja katika jamii yetu na kuwapa elimu ya uelewa kuhusu utaratibu ambao unatumika katika kuhamisha makaburi. Kwa kufanya hivi inasaidia kuondoa migogoro baina ya serikali na wananchi wake. Nitoe wito kwa viongozi na wananchi waendelee kutoa ushirikiano katika zoezi hili na hatimaye kazi iendelee," alisema.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Majengo wilayani Manyoni, Hassan Simba, alisema: "Sisi viongozi wa maeneo haya tunaahidi kutoa ushirikiano kwa TRC na mkandarasi katika shughuli zote za mradi zinazoendelea katika kata yangu. Reli hii ikikamilika itarahisisha shughuli za kijamii na kilimo kwa wakazi wa Manyoni."

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Itigi, Chiristopher Kiwango, akizungumza kwa niaba ya viongozi wa dini, alishukuru TRC na serikali ya wilaya kwa namna jambo hilo lilivyoendeshwa kwa kuzingatia taratibu za haki na sheria za binadamu, misingi ya imani pamoja na uzingatiaji wa afya wakati wa kuhamisha makaburi.

"Tunaishukru serikali ya Tanzania kwa kutupa viongozi waliosimamia zoezi hili kubwa ambalo limefanyika kwa utaratibu uliozingatia mambo ya afya, imani za marehemu pamoja na haki za binadamu. Tunamshukuru Mungu lakini pia shukrani ziende kwa wale wote walioshiriki katika kazi ya kuhamisha makaburi," alisema.

"Katika utekelezaji wa ujenzi wa SGR ni kweli kwamba maeneo mengi ya wananchi yametwaliwa na TRC kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli ya kisasa. Hata hivyo, TRC imekuwa ikitwaa ardhi kwa kuzingatia sheria na kanuni za ardhi ikiwamo malipo ya fidia na kifuta machozi ambazo ni haki kwa waathirika hao wa mradi," aliongeza.

Baada ya kuhamisha makaburi TRC inaendelea na utaratibu wa ulipaji wa kifuta machozi kwa wananchi ambao ni wasimamizi wa makaburi ya ndugu zao yaliyohamishwa kwa lengo la kumpisha mkandarasi kuendelea na ujenzi.


**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

**UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA AJIRA ZA MUDA KWA KAYA ZA WALENGWA**

Miradi ya ajira ya muda kwa walengwa wa TASAF ni utaratibu wa utekelezaji miradi ya jamii yenye kutumia nguvu kazi, inayoshirikisha walengwa kufanya kazi na kulipwa ujira. Miradi hiyo inawezesha jamii kupata rasilmali /miundombinu inayotoa huduma na ujuzi kwa jamii kupitia ushiriki wao katika kutekeleza miradi hiyo.

Washiriki wa kazi zinazotoa ajira ya muda kwa walengwa ni watu wenye uwezo wa kufanya kazi wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 65. Kila kaya ambayo inashiriki katika ajira za muda kwa walengwa inaandikisha watu wawili, ambapo mtu mmoja kutoka kwenye kaya ndiye atashiriki kazi kwa wakati mmoja. Utekelezaji wa miradi ya ajira ya muda huchukua miezi sita ambapo walengwa hufanya kazi kwa siku kumi tu kwa kila mwezi. Kwa siku mlengwa anatakiwa kufanya kazi kwa muda usiozidi masaa manne ili aweze kupata muda wa kufanya shughuli nyingine.

Wazee, watu wenye ulemavu, wakina mama wajawazito na wenye watoto wadogo ambao hawajatimiza miaka miwili hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira za muda kwa walengwa. Wasimamizi wanaopanga kazi za walengwa hawatakiwi kuwapangia kazi watu hao na wanapaswa kutoa taarifa kwa wajumbe wa kamati ya usimamizi wa mradi (CMC) na Waratibu ili majina ya watu hao yaondolewe kwenye orodha ya watu walioandikishwa kufanya kazi za ajira ya muda. Kaya yenye watu ambao hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira ya muda watapokea ruzuku ya msingi.

Uongozi wa TASAF umetoa waraka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Ufuatiliaji kupitia orodha za watu walioandikishwa kufanya kazi kwenye miradi ya ajira za muda na kuwaondoa wale ambao hawaruhusiwi kufanya kazi kwenye miradi hiyo. Aidha utoaji wa elimu kwa viongozi wa jamii, wasimamizi na walengwa kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa kaya za walengwa utaendelea kutolewa katika kipindi chote cha utekelezaji.

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF**

217333102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyabiashara hiki ni kipindi cha kupata thawabu

**WAKATI** Waislamu nchini wakianza mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, viongozi mbali mbali wa serikali na dini wamewataka wafanyabiashara kutopandisha bei za bidhaa hasa za vyakula ili kuwawezesha wafungaji kumudu kununua.

Rai hiyo ya viongozi hao inatokana na mazoea ya kila inapofika kipindi cha mfungo, wafanyabiashara kukitumia kama cha kupatia faida.

Bei za vyakula sokoni na madukani hupanda ghafla na kuwafanya wanaofunga kushindwa kumudu gharama za vyakula vya futari na kuishia kula ugali au wali.

Watu wanapofunga kutwa nzima na jioni wanapofungua vinywa wanatakiwa kuanza na vyakula laini kama inavyoshauriwa na wataalam wa afya kwa kuzingatia mlo unaotakiwa. Vyakula vinavyopendwa wakati wa mfungo ni aina ya nafaka kama maharage, kunde, ngano na vile vyenye asili ya mizizi kama mihogo, magimbi na viazi vitamu na vingine vinavyopendwa kuliwa wakati huo.

Hata hivyo, inapofika kipindi hiki cha Ramadhani, bidhaa hizo ambazo hazionekani kwa wingi sokoni kipindi cha kawaida, huanza kuibuka na bei zake huwa hazishikiki.

Inavyoonekana baadhi ya wafanyabiashara huamua kuziweka pembeni wakisubiri kipindi hiki ambacho huhitajika kwa wingi na kuzimwaga sokoni kwa ajili ya kupata faida kubwa. Vyakula ambavyo huonekana kwa wingi wakati wa mfungo ni maboga, mihogo na vile vinavyotokana na bidhaa zitokanazo na nafaka ya ngano.

Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi, aliwaonya wafanyabiashara visiwani humo tabia ya kupandisha bei ya vyakula kipindi cha mfungo kwa kuwa hawawatendei haki wanaotafuta thawabu kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwafanya washindwe kununua bidhaa.

Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir, pia alikemea tabia hiyo na kuwaasa wafanyabiashara kuwa ni vema kipindi hiki cha mfungo wakawaonea huruma wale wanaofunga kwa kushinda na njaa na kuwafanyia wepesi wanapofungua ili wafanyabiashara hao wapate thawabu kwa Mwenyezi Mungu.

Kipindi hiki cha mfungo ambacho waumini wa dini za Kikristo (walioanza mfungo wiki tatu zilizopita) na Waislam walioanza jana ni cha kuomba toba kwa Mungu ili waweze kusamehewa dhambi zao.

Pia, kipindi hiki watu wengi hufanya mema kwa kuwakumbuka wenye shida kama za ugonjwa, wasiokuwa na uwezo kimaisha na wenye uhitaji kwa kuwapa misaada ili nao wanaposhukuru kwa misaada hiyo, watoaji wanapata baraka.

Kipindi hiki ambacho watu wanatakiwa kutenda matendo mema ni vema kila mtu akakitumia kufuta madhambi yake ya nyuma kwa kurudisha mema kwa Mwenyezi Mungu.

Vivo hivyo kwa wafanyabiashara wanatakiwa kutenda mema kwa kuwahurumia wenzao wanaofunga kwa kuuza bidhaa zao kwa bei halali na hata ikiwezekana wasiangalie kupata faida kubwa kwa kuwaumiza wanaonunua. Mungu huwalipa wanaotenda mema kwa njia nyingi.

Unaweza ukatenda jambo jema leo, lakini ukarudishiwa wema wako baadaye ukiwa umeshasahau kuwa ulimtendea mtu jambo jema.


Hivyo, kipindi hiki kitumike kwa watu wote kutenda mema ili kila mtu afurahie kufunga wakati akitubu kwa yale aliyoyatenda ambayo hayakumpendeza Mungu.

Mtu anapofunga huku moyoni akiwa na masikitiko au akiwaza atakula nini ni sawa na kushinda na njaa.

Tunawatakia mfungo mwema Waislam wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tumeanza kujisahau tunachangia maji, ila kifua kikuu na Ukimwi havijatusahau

Na Adam Fungamwango

**NI** ukweli usiopingika kuwa baadhi ya magonjwa nchini kwetu yameanza kupungua kasi ya kuenea, kutokana na elimu inayotolewa na kuwafikia wananchi, pamoja na serikali kutekeleza wajibu wake kwa raia.

Serikali ya Tanzania imefanya kazi kubwa, si kwenye kuelemisha tu, bali hata kutoa dawa na kutelekeza wajibu wake wa kuwafikia wagonjwa kwa wakati.

Magonjwa ya kuambukiza kama ukimwi, kifua kikuu, homa ya ini na mengine yanayofanana, kwa sasa si kubwa sana, kama ilivyokuwa miaka zama kurudi hadi 2000 mpaka 1990.

Zamani wakati maambukizi ya Ukimwi yamepamba moto, kulikuwapo elimu inayosema, si tu kwamba wanaoambukizwa wanavipata virusi kwa ajili ya uasherati, au ngono zembe, pia mtu anaweza kuupata kwa kuchangia nyembe, vyombo vya kutogea, hata kuchangia miswaki.

Hilo likawafanya watu wengi kuwa makini, kiasi kwamba ilifika hatua waliogopa hata kwenda saluni kunyoa na mashine zinazotumia umeme, kwa madai wanaweza kuambukizwa,mpaka pale wataalamu walipothibitisha si hivyo.

Nyenzo hizo zinakuwa na joto kali la umeme, wakasisitiza usafi wa mashine hizo kwa dawa ambazo zinapatikana kwenye saluni sasa.

Ni kipindi ambacho ilikuwa vigumu kuona hata wanandugu wakichangia maji, soda au juisi kwenye chupa moja. Ukiona wanafanya hivyo, basi angalia, utakuta ni wa jinsia mbili tofauti na wana uhusiano wa kimapenzi au wanandoa.

Nadhani baada ya ugonjwa huo kupungua kasi yake, elimu nayo pia imepunguzwa kutolewa, kwa maana ya umma sasa unajitambua.

Inatakiwa kwa sasa, kufahamu kwamba, ili mtu kupata maambuziki ya virusi vya Ukimwi, lazima tu ufanye ngono zembe na njia nyingine zembe ya kuambukizana .

Kibaya sasa, kumeibuka kasi ya watu kuchangia chupa moja ya maji, soda na juisi. Nimekutana na hili sehemu nyingi sana kwa siku za karibuni. Vijana sokoni, vijiweni, kinadada saluni, madereva na makonda, huko kote unakuta watu wanachangia chupa moja.

Mmoja anaweza kununua chupa ya maji, anakunywa halafu anamuachia mwenzake. Naye anaingiza mdomo kwenye chupa hiyo hiyo.

Siyo chupa tu, hata vikombe kwa sasa watu wanashea tu bila woga, kama ile miaka ya nyuma kabla magonjwa hayo hayajaingia.

Hiy0 ni hatari sana kwa sababu inaweza kabisa ikasababisha maambukizo ya ukimwi kurudi tena kwa kasi. Kuambukizwa virusi vya ukimwi kwa kuchangia chupa, vikombe, miswaki, nyembe ni rahisi zaidi kuliko hata kuvipata kwa njia ya kujamiiana.

Kwa sababu hapa wanaambukizwa watu wengi kwa muda mfupi tu, wakiachiana kunywa maji, soda, au juisi.

Mbali na ugonjwa huo, lakini kuchangia vikombe, au chupa kunasababisha maambukizo pia ya ugonjwa wa kifua kikuu.

Magonjwa kama Ukimwi, kifua kikuu, ugonjwa wa ini, yanaambukizwa kwa damu, mate, makohozi ambayo yanaweza kutoka kwa mgonjwa na kwenda kwa mtu mwingine ambaye si mgonjwa naye akaupata.

Mfano ni mtu ana virusi vya Ukimwi na mdomo wake ukawa umechubuka na unatoa vitone vidogo vya damu, akinywa maji na kumpa yeyote yule, anayekunywa anaweza kuupata kwa kukutana na vitone vile ambavyo ama vitakuwa ndani ya maji, au kwenye mdomo wa chupa.

Kwenye ugonjwa wa kifua kikuu ndiyo rahisi zaidi kwani mate tu yaliyochanganyikana na vitone vya makohozi yanaweza kutoka kwa mgonjwa huyu kwenda kwa mwingine kama mgonjwa huyo hajaanza kunywa dawa.

Serikali inatumia gharama kubwa kuponyesha wagonjwa na kuzuia magonjwa hayo yaendelee kuelea, hivyo Watanzania kuna haja kuanza kukumbushana kuacha tabia ya kuchangia chupa moja ya maji kwa mtu zaidi ya mmoja.

Watu wakitaka hivyo, basi kabla mmoja hajanywa, amiminie wenzake kwenye glasi au vikombe na yeye aendelee, lakini siyo kupeana kila mmoja anaweka mdomo wake kwenye chupa hiyo hiyo moja, kitu ambacho ni hatari sana.

Narudia kusema kuwa ugonjwa wa ukimwi bado upo, na kifua kikuu bado kipo hivyo tuendelee kuchukua tahadhari na kuwakumbusha vijana wa kizazi hiki kuwa wawe waangalifu kwani hata kushea chupa za maji, soda juisi wanaweza kujiingiza kwenye hatari ya kupata maambukizi pia.

## HakiElimu yalaani adhabu kubwa iliyomsababishia kifo mwanafunzi

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya HakiElimu, imelaani adhabu iliyotolewa kwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mwinuko ya jijini Mwanza, Gloria Faustine (14), ambayo ilisababisha kifo chake.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi Dar es Salaam, Kalage alisema ni vema adhabu zinazotolewa kwa wanafunzi zizingatie aina ya kosa na ziwe ni zile zenye kuwasaidia kuwa bora zaidi na si vinginevyo.

Alisema kuwaadhibu wanafunzi kwa sababu za kitaaluma kama kushindwa kuzungumza lugha ya Kiingereza, kuandika na kukokotoa hisabati hakuwezi kutatuliwa kwa kuwapa adhabu.

"Tunatambua kuwa walimu wana jukumu la kuwafundisha na kuwajenga wanafunzi katika mwenendo unaofaa, hata hivyo jukumu hilo wanaweza kulitekeleza kwa kutumia mbinu mbalimbali za adhabu chanya za kufikia malengo ya utoaji adhabu,"alisema Dk.Kalage.

"Tunapenda kusisitiza kuwa adhabu zitolewazo kwa wanafunzi ni lazima zizingatie aina ya kosa au tabia inayokusudiwa kurekebishwa na zilenge katika kumsaidia mtoto kuwa bora zaidi  badala ya kumuumiza na kumwongezea hofu."

Alisema matukio kama hayo ya adhabu zinazoleta matokeo hasi kwa wanafunzi yanazidi kuongezeka na kuibua hofu kwa wanafunzi na wazazi.

"Kwa mfano katika mazingira hayo badala ya adhabu aliyoitoa mwalimu, angeweza hata kuagiza wanafunzi waandike insha ya lugha ya Kiingereza, kusoma vitabu vingi vya hadithi za lugha hiyo na kutoa tafsiri, kutafuta misamiati kadhaa na kuitumia katika sentensi au kuandaa mijadala ya lugha hiyo na kila mtu ashiriki, adhabu kama hii ingewasaidia zaidi wanafunzi kujifunza lugha hiyo."

Kutokana na matukio hayo kuendelea, Dk.Kalage aliiomba serikali kurejesha upya mapendekezo yanayotolewa na wadau kuhusu matumizi ya lugha ya kiswahili kama lugha ya kufundishia ngazi ya sekondari.

"Ni wazi kuwa watoto wanaotoka shule za msingi na hasa za umma kuingia kidato cha kwanza wanakuwa hawajawa tayari kutumia lugha hiyo ya Kiingereza katika kuzungumza na kujifunzia. Kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia sekondari itatoa fursa kwa watoto kujifunza kwa ufasaha na kufundishwa vema Kiingereza na lugha nyingine za kigeni,"alisema.

Alisema moja ya malengo yanayobainishwa kwenye mtaala wa sekondari wa mwaka 2005 toleo la mwaka 2013 ni kumwezesha mwanafunzi kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya kiswahili.

Gloria alifariki kutokana na kuangukiwa na jiwe wakati akichimba kifusi kama sehemu ya utekelezaji wa adhabu aliyopewa pamoja na wenzake kwa kosa la kuzungumza lugha ya kiswahili katika mazingira ya shule.




Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Jerry Silaa (katikati), akizungumza kuhusu uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya umeme, walipotembelea kituo cha kuzalisha na kusambaza umeme wa kilovoti 33/11 cha Bangwe, Kigoma mjini mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lataka mpango kunusuru Posta, TTCL

**Na Mary Geofrey**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imeitaka serikali kuharakisha mpango wa kuzinusuru taasisi za umma zenye madeni makubwa, ili ziweze kujitegemea na kujiendesha kibiashara.

Miongoni mwa mashirika yaliyotajwa na kamati hiyo kuwa na madeni makubwa ni Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL).

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Moshi Kakoso alitoa agizo hilo mapema wiki hii, Dar es Salaam wakati kamati hiyo ilipotembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Alimwagiza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (pichani), kuharakisha mchakato huo ili kuhakikisha mashirika hayo yanajisimamia na kujiendesha kwa faida.

"Serikali ihakikishe madeni makubwa yatafutiwe muafaka yakiwamo ya TTCL na Shirika la Posta wana madeni kiasi cha kushindwa kukopesheka. Serikali inaweza mkasaidia kama yapo mnayoweza kuyabeba muyabebe, mnayoweza kuyabadili kuwa mtaji mfanye hivyo ili yakidhi vigezo vya kujiendesha," alisisitiza Kakoso.

Aidha, aliagiza TTCL iwezeshwe kuendesha mkongo wa Taifa kibiashara na kuiingizia serikali mapato ya kutosha na kuleta manufaa makubwa kwa nchi.



Kakoso pia alipendekeza wizara kuongeza bajeti ya fedha kwa Shirika la Utangazaji (TBC) Idara ya Habari Maelezo na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), ili kujiendesha kwa faida.

Katika hatua nyingine aliipongeza wizara hiyo kwa juhudi kubwa za kusimamia taasisi zake na kusaidia Taifa kuendelea kukua katika sekta teknolojia na mawasiliano.

Kwa upande wake Waziri Nape, aliahidi kufanyia kazi maagizo yote ya kamati kwa maslahi mapana ya Taifa.

Alisema madeni hayo yote ya taasisi mbalimbali zilizopo chini ya wizara hiyo yapo kwenye mpango wa kuyalipa.

Alisema watasafisha vitabu vyao ikiwamo kuchukua madeni yao kuwa mitaji ili kujiendesha kibiashara.

"Yanahakikiwa tayari tumeshachukua namba kwa ajili ya kuanza kulipwa na mengi ni ya muda mrefu sana, hivyo lazima tusafishe vitabu vyao ili kujiendesha kwa faida," alisisitiza Nape.

Kamati pia ilitembea mtambo wa kuchapisha magazeti ya umma ambao uliwasili nchini juzi tayari kwa ajili ya kufunza na kuanza kufanya kazi.

## KABWELA



HABARI KITAIFA

# Wawezeshwa kukabiliana na mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Dk. Omary Nkullo, amezindua mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wanawake wa vijijini wilayani humo.

Mradi huo unaojulikana kama Rural Women Climate Change Adaptation (RUWOCCA) unatekelezwa na asasi ya Environment Media Agenda (EMA) kwa ufadhili wa Mfuko kwa Wanawake wa Afrika (FMxA) kutoka Hispania.

Akizindua mradi huo juzi, Dk. Nkullo alihimiza kinamama hao kusajili vikundi vyao ili kunufaika na mikopo ya halmashauri kuboresha miradi yao ya ufugaji nyuki.

Mradi wa RUWOCCA unanufaisha zaidi ya kinamama 100 kwa ajili ya upandaji miti kuni, kivuli na matunda, ufugaji nyuki na utumiaji wa majiko banifu.

Akikabidhi mizinga ya nyuki kwa wanavikundi na baadaye kutembelea kitalu cha miche, Dk. Nkullo alisema halmashauri yake inafarijika kuona jitihada za EMA katika kuwawezesha wanawake kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kwamba wako tayari kushirikiana na EMA kuhakikisha mradi wa RUWOCCA unafanikiwa na kuleta mabadiliko ya maisha bora kwa wanawake wa wilaya ya Kongwa.

Akizungumzia juu ya upandaji miti, Dk. Nkullo alisema Kongwa ina mkakati wa kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka huu na kwamba miche 5,500 iliyotayarishwa hadi sasa na mradi wa RUWOCCA itasaidia kufikisha lengo la wilaya la kupanda miti ikiwa ni mkakati wa kukijanisha mkoa wa Dodoma.

Mwenyekiti na mwanzilishi wa EMA, Secelela Balisidya, alimshukuru mkurugenzi huyo na serikali kwa ujumla kwa kutambua na kuthamini mchango wa asasi zisizo za serikali katika kuwaletea wananchi wa Tanzania maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa EMA, Balbina Makoi, amesema Wilaya ya Kongwa ilichaguliwa kutekeleza mradi huo kutokana na jiografia na hali yake ya ukame na mvua chache.

Aliwataka wanufaika wa mradi kufanya kazi kwa bidii kutekeleza mradi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoleta athari nyingi nchini na duniani kote.

Naye Mratibu wa RUWOCCA, James Nkini, aliwashukuru wanawake waliojitokeza kutekeleza mradi huo na kubainisha kuwa ni dhahiri mabadiliko yataonekana katika maisha yao hasa katika kujiongezea kipato kwa kuuza asali pia kujipatia kuni kutokana na miti watakayoipanda pembezoni mwa nyumba zao, hivyo kupunguza kutembea umbali mrefu kutafuta kuni.

Ofisa Mradi wa RUWOCCA, Nyemo Sawasawa, aliwahimiza kinamama kujitokeza wakati wa mafunzo mbalimbali yatakayokuwa yanatolewa juu ya ufugaji nyuki, na jinsi ya kujenga majiko banifu ili kujijengea maarifa na kukuza stadi za maisha yao.

RUWOCCA ni mradi wa 12 kutekelezwa na asasi ya EMA tangu ilipoanzishwa mwaka 2008.

Mwaka huu, EMA inasherehekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwake, ikihesabu mchango wake kwa jamii ya Tanzania kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhifadhi, kusimamia na kutunza mazingira na hasa ile ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja (wa pili kulia), akishuhudia utiaji saini wa ujenzi wa mradi wa kuchakata majitaka eneo la Mbezi Beach kati ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) na mkandarasi Kampuni ya Metito (Overseas) Ltd ya Dubai, jana. Mradi huo, utaweka historia ya uchakataji majitaka nchini kwa kuwa na mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kuchakata lita milioni 16 za majitaka kwa siku. Kulia ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Kijiji chawa mfano matumizi bora ardhi

**Na Munir Shemweta,** HANDENI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema Kijiji cha Msomera kilichoko Handeni mkoani Tanga, kitakuwa cha mfano kwa vijiji vingine nchini kwenda kujifunza kutokana na kuwekewa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kusimamiwa vizuri.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati wa kukabidhi hati miliki za ardhi kwa wananchi waliohamia kijiji hicho kutoka Ngorongoro mkoani Arusha pamoja na wenyeji, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

"Kijiji hiki sisi kama serikali tunakwenda kukifanya kuwa cha mfano maana yake watu watatoka maeneo mengine kuja kujifunza hapa kutokana na kilivyopangwa na mnavyoisimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Mabula, wananchi waliopelekwa katika kijiji hicho hawakuhamishwa kwa bahati mbaya bali ni dhamira na nia njema ya serikali kumwezesha Mtanzania mmoja mmoja.

"Wote tunajua kabisa nia ya serikali ni njema. Kitendo cha kuletwa na kuwa na uhakika wa ardhi kwa ajili ya kujenga na kupewa ardhi kwa ajili ya kilimo kwa ekari tano kwa kila kaya ni jambo la kumshukuru Mungu na Rais wetu, Samia Suluhu Hassan," alisema Dk. Mabula.

Aidha, Dk. Mabula aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuepuka migogoro kwa kuwa Msomera ni eneo ambalo serikali inalitupia macho na kujifunza. Alisisitiza kuwa wizara haitaki kuona panakuwa na vijiji vinavyokua bila mpangilio.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Prof. Wakuru Magigi, alisema awamu ya kwanza ya utekelezaji mradi kwenye kijiji cha Msomera, serikali imejenga takriban nyumba 503 na viwanja vilivyopatikana eneo hilo yaani kupangwa na kupimwa ni 4,620 huku viwanja 14,570 vikiwa vimebuniwa.

Prof. Magigi alisema katika viwanja hivyo kuna maeneo ya huduma mbalimbali vikiwamo viwanja vya makazi kila kimoja kikiwa na ukubwa wa ekari 2.5 lakini wakati huo huo kukiwa na maeneo ya mashamba yenye ukubwa wa ekari tano. Maeneo hayo yanagawiwa kwa wananchi wanaohamia na wenyeji.

# Wakazi 4,000 wanufaika huduma ya majisafi

**Christina Haule,** MOROGORO

ZAIDI ya wakazi 4,000 wa vijiji vya Kobogoji na Pandambili, Mvomero mkoani hapo wameanza kunufaika na mradi wa maji unaogharimu Sh. milioni 530 unaojengwa kupitia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoani Morogoro.

Wakizungumzia mradi huo juzi wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kimkoa wilayani Mvomero wakati Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa, akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo ulioko Turiani, wananchi hao waliishukuru serikali kwa kuwasaidia kupatikana kwa huduma ya maji ambayo waliikosa tangu kuanzishwa vijiji hivyo.

Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Kibogoji, Asha Mashaka, alisema walilazimika kuibua mradi huo ulioanzishwa kwenye kijiji cha Kibogoji kutokana na adha ya maji waliyoipata ambayo iliwafanya kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kutafuta maji huku wakiacha shughuli za uzalishaji.

Mashaka alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwasaidia kupata maji na kwamba kukamilika kwa mradi huo kumewaondolea adha ya kutumia muda mwingi kuteka maji katika mabwawa na visima vya kunyweshea mifugo jambo ambalo ni hatari kwa afya hasa kwa watoto.

Awali, Kaimu Meneja wa RUWASA Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Sospeter Lutonja, alisema mradi huo wa ujenzi wa tangi la maji na usambazaji, umegharimu Sh. milioni 530 huku ukiwa umekamilika kwa karibu asilimia 95 na unatarajia kunufaisha wakazi 4,251 wa vijiji hivyo.

Mhandisi Lutonja pia alisema katika kuendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini, RUWASA inatarajia kutumia zaidi ya Sh. milioni 200 kwa mwaka wa fedha 2023/24 kuboresha miundombinu ya miradi ya maji katika maeneo mbalimbali.

Alisema maboresho hayo ya miundombinu ya maji yanafanywa kutokana na uharibifu unaochangiwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji ikiwamo kilimo na mifugo.

Aidha, alisema pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji, wamekuwa wakitumia gharama kubwa kuboresha miundombinu iliyoharibiwa, hivyo kuwataka wakazi hao kuona haja ya kuwa walinzi wa kwanza wa miundombinu hiyo ili kuleta tija inayokusudiwa huku wakikumbuka kauli ya wahenga inayosema 'kitunze kikutunze'.

Naye Mwassa aliwataka wakazi wa vijiji hivyo kuhifadhi na kulinda miundombinu na vyanzo vya maji vilivyoko na kwamba kama wataharibu, wasitegemee kupata huduma hiyo kila mara bali itahamia kwa wengine.

# Wakulima watuhumiwa kuihujumu chemchemi ya Kinamiri

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAKULIMA wakubwa na wenye uwezo kifedha wanatuhumiwa kuihujumu chemchemi ya Kinamiri iliyoko Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro wakidaiwa kuziba mlango wa maji ya umwagiliaji kwa viroba vya mchanga ili yasiende kwa wakulima wadogo wa vijiji vya Kawaya, Longoi Nguzo Nne na Ngosero.

Vijiji hivyo vyenye wakulima zaidi ya 20,000 vinategemea chanzo hicho kulima mazao ya vitunguu, nyanya, mahindi, maboga lishe, mahindi na bamia kwa ajili ya kujipatia kipato.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana katika mkutano uliofanyika Kitongoji cha Mapacha na Ngosero, baadhi ya wakulima waliopoteza mazao yao kutokana na kukosa maji, akiwamo Mbonea Elienezer, alisema tatizo hilo limesababishwa na wakulima wakubwa wa mpunga waliovamiwa chanzo hicho na kukigeuza kuwa mashamba. Alisema: "Skimu yetu ilikuwa na uwezo wa kumwagilia ekari 200 ambayo skimu hii inahudumia watu zaidi ya 1,200 lakini cha kusikitisha pameingia matajiri wachache ambao wamehujumu chanzo cha Mto Kinamiri".

Aliongeza: "Kwa hiyo ufanisi wa kilimo cha umwagiliaji umeshindwa katika vijiji vitatu vyenye watu zaidi ya wanachama 70,000 na watu wanaotegemea hicho chanzo ni wengi lakini wanaohujumu hawafiki watu 30." Apolkaria Mlacha, ambaye ni mkulima wa mahindi, mboga na vitunguu wa Kawaya alisema kutokana na tatizo hilo wamepata hasara ya anguko la kiuchumi.

Mkulima mwingine, Eva Adolph, alisema licha ya kununua mbolea ya ruzuku imekuwa ikiishia shambani bila tija, huku pia wakishindwa kurejesha mikopo ya asasi za fedha, hivyo wanaiomba serikali isikilize kero ya wakulima wadogo.

Alipotafutwa kuzungumzia malalamiko hayo, Ofisa Umwagiliaji wa Wilaya ya Hai, Msafiri Msuya, alikiri ni kweli wananchi hao walishafika kwenye ofisi yao na kama serikali walianza kuchukua baadhi ya hatua. Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Bonde la Mto Pangani (PWBO), Segule Segule, alisema chemchemi ya Kinamiri imekuwa ikikumbwa na tatizo la kupungua kwa maji.

"Nimelipokea kama mgogoro au changamoto ambayo haijatatuliwa na tumeshajipanga watu wangu wiki hii wanaenda huko kushughulikia tatizo hilo," alisema.

Segule alisema: "Chini ya uratibu wa Jumuiya ya Watumia Maji walikubaliana wapunguziane maji na wakaweka zamu itakayowezesha maji kufika ukanda wa chini, ambako kuna mifereji ya Longuo A, Longuo B, lakini wenye tatizo kubwa ni huo wa Longuo A".



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani (kushoto), akitembelea shamba la miti linalomilikiwa na kikundi cha jamii cha Kisito wilayani Kasulu, mkoani Kigoma mapema wiki hii, ambalo limepandwa na kutunzwa kwa ufadhili wa kampuni ya tumbaku ya Alliance One. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Uzalishaji wa kampuni hiyo, David Mayunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo wa mshitiri waanza kutoa matunda sekta ya afya

**Na Hamida Kamchalla**, TANGA

SERIKALI mkoani Tanga imesema uboreshaji wa huduma za afya na utoaji wa afua mbalimbali unatoa matumaini kwamba mfumo wa mshitiri unaotumika hivi sasa una uhakika wa asilimia 100 wa upatikanaji wa bidhaa za afya.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Georde Mmbaga, aliyesema hayo juzi wakati akizindua mafunzo ya wawezeshaji wa mfumo wa mshitiri, ambao wanajengewa uwezo ili kupata wawezeshaji wa ngazi ya mkoa na halmashauri za wilaya. "Mfumo huu unawezesha upatikanaji wa bidhaa za afya, ambazo zinakosekana katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD). Tunafanya hivi ili kuimarisha na kurahisisha vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

Zaidi aliongeza: "Serikali imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za afya unakua kwa asilimia 100, ikiwemo mfumo huu wa mshitiri.

"Sisi kama viongozi tuna jukumu la kuvisimamia vituo ili viweze kukusanya mapato ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya, sambamba na kusimamia mnyororo wa ugavi wa bidhaa hizo." Mmbaga alisisitiza katika mafunzo hayo washiriki ambao ni wahudumu wa afya watajifunza utekelezaji wa mfumo wa mshitiri kwa kupitia mwongozo wa utekelezaji wa mfumo huo pamoja na mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa.

Aidha, Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, Mkoa wa Tanga, Dk. Rehema Majid, alisema mafunzo hayo yameshirikisha halmashauri zote za Mkoa wa Tanga, kwamba kupitia mfumo huo hakutakuwa na upungufu wa bidhaa za afya.

Vilevile Dk. Majid alisema mfumo huo utaondoa malalamiko ya wananchi katika vituo vya kutolea huduma za afya.

# Wanaoishi jirani Hospitali ya Kibong'oto watolewa hofu

**Na Anjela Mhando,** SIHA

HOSPITALI ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto, imewatoa hofu wakazi wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, ambao makazi yao yamepakana na maabara ya kisasa yenye uwezo wa kupima virusi kwamba hawawezi kupata maambukizi yanayotokana na vimelea vya magonjwa tishio yanayoibuka.

Maabara hiyo ni ya mfano Afrika katika kuchunguza virusi na bakteria kwa kiwango cha vinasaba.

Jana, Mtafiti wa Magonjwa Ambukizi wa Hospitali hiyo, Dk. Peter Mbelele, akizungumza na wajumbe wa serikali ya Kijiji cha Mae, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Ivaeny na viongozi wa dini, alisema maabara hiyo hairuhusu vimelea kutoka nje ya jengo hilo.

"Kukamilika kwa maabara ya afya ya jamii ngazi ya tatu ya usalama iliyoko kwenye hospitali yetu, itachangia katika udhibiti wa kusambaa kwa magonjwa duniani na hivyo kuimarisha uchumi na usalama wa binadamu,"alisema Dk. Mbelele.

Aidha, Dk. Mbelele, aliwaeleza wananchi hao kuwa serikali imewekeza Sh. bilioni 12.5 kwa ajili ya kujenga maabara hiyo, lakini imetoa Sh. bilioni 10 za kununua mitambo iliyofungwa kwenye jengo hilo.


Vilevile, Dk. Mbelele, alisema maabara hiyo itafanya ufuatiliaji wa usugu wa vimelea kwa dawa zinazotumika kwenye matibabu ya magonjwa mbalimbali na kufanya tathmini ya kiwango cha dawa mwilini.

Pamoja na mambo mengine, maabara hiyo itafanya pia utafiti kuhusu ubunifu katika sayansi ya tiba na kinga katika ugunduzi wa dawa, vitendanishi, vifaa tiba na kutengeneza chanjo mbalimbali za kuzuia na kukinga magonjwa ambukizi.

Alisema Hospitali ya Kibong'oto, itatunza vimelea vya magonjwa mbalimbali ikiwamo vinasaba vya vimelea, kutoa mafunzo ya kiuchunguzi na ubunifu, kwa wataalamu katika sekta ya afya.

Meneja wa Maabara hiyo, Dk. Shaban Mziray, aliwatoa hofu viongozi hao kwamba mitambo na vifaa vilivyowekwa katika jengo hilo iko kwenye uangalizi mkubwa.

Diwani wa Ivaeny, Elinisaa Kileo, alimshukuru mtafiti huyo kwa kuwatoa hofu wananchi.





# 400 wajitokeza kupata matibabu, uchunguzi wa macho

**Na Neema Sawaka,**
KAHAMA

WANANCHI 400 kutoka Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga wamejitokeza kwenye kliniki ya huduma ya uchunguzi, matibabu ya macho.

Kati ya idadi hiyo, 15 walipatiwa huduma ya upasuaji kutoka kwa madaktari bingwa kwa muda wa siku tatu.

Hayo yamebainishwa juzi na Daktari Bingwa kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Christopher Mwanasao, wakati wa utolewaji wa huduma hiyo ambayo ilifadhiliwa na Serikali ya Ujerumani.

Mwanasao alisema idadi ya watu wanaopata shida ya kuona wanaongezeka kila siku kutokana na matumizi ya nishati ya mkaa pamoja na kuni hususani katika maeneo ya vijijini.

"Kufanya kazi sana nayo ni moja ya matatizo ya kupata shida kwenye macho na suala la utumiaji wa simu za mkononi na kompyuta hilo halihusiani moja kwa moja na matatizo ya macho," alisema Mwanasao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Philipo Nyaga, alisema kliniki ya macho ipo kila siku ila jamii imezoea kufika kwa wingi siku maalumu iliyotengwa.

Baadhi ya wananchi waliofika kupata huduma ya macho na upasuaji katika hospitali hiyo walisema ujio wa madaktari bingwa umekuwa neema kwao, kwamba wamefanyiwa upasuaji na matibabu ya macho kwa gharama nafuu.

Mmoja wa wakazi hao, James Magadula alisema: "Huduma hii inatufanya kuondokana na tatizo la kusaka huduma za kibigwa kwenye hospitali za rufani kwenye mikoa ya Mwanza na KCMC Moshi".




Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Barrick Gold Corporation, Mark Bristow (kushoto), akishirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, kukata utepe wakati kampuni hiyo ilipokabidhi msaada wa gari la kubeba wagonjwa katika Kituo cha Afya Bugarama wilayani Msalala mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yabaini ubadhirifu kivuko cha Kigongo-Busisi

**Na Vitus Audax**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mwanza imebaini ubadhirifu katika Kivuko cha Kigongo-Busisi unaotokana na kuchezewa kwa mitambo ya ukaguzi, matumizi ya risiti pamoja na ukwepaji kodi kwa baadhi ya magari.

Hayo yamebainishwa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mwanza, James Ruge, wakati akitoa taarifa ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha miezi mitatu.

Alisema kuwa baadhi ya magari yamekuwa yakipitishwa bila kulipia ushuru kwa kigezo kuwa ni magari ya wakubwa (viongozi), hivyo hayapaswi kulipia.

Alieleza kuwa miongoni mwa mambo yanayofanywa na watumishi katika kivuko hicho ni pamoja kutokukagua magari yanayofahamika kama VIP, hivyo yanapita bila kulipa mapato, kuchezea mitambo ya ukaguzi wa tiketi na kufanya tiketi hizo kuuzwa zaidi ya mara mbili.

Alisema pia walibani magari ya watu binafsi kupita bila kulipia yakidaiwa kuwa ni magari ya serikali.

Vilevile alisema pia kuna watu wasio maalum (vishoka) wanakatisha tiketi kinyume na miongozo ya kiutendaji, hivyo kuwataka kusitisha shughuli hizo na kuwahimiza watumishi wote kuzingatia miongozo iliyopo kuhusiana na mizani ili magari yote yaweze kulipiwa tozo na kuondoa hujuma.

# DC alalamika utaratibu wa kuwashtaki wezi vifaa vya SGR

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita, amelalamika utaratibu wa kuwapeleka watuhumiwa wa wizi wa vifaa vya mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Mwanza-Isaka, Isaka-Tabora kufunguliwa mashtaka katika mahakama za Jiji la Mwanza.

Aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya kushtukiza katika moja ya kambi ya ujenzi wa SGR na kusema hali hiyo inasababisha kudidimiza juhudi za kutokomeza vitendo hivyo vya wizi.

Mhita alisema watu wanaokamatwa wakiiba vifaa katika mradi huo wamekuwa wakipelekwa jiini Mwanza kwa ajili ya kushtakiwa.

Hivyo, alilitaka Jeshi la Polisi kuwafikisha watuhumiwa hao katika mahakama zilizoko maeneo husika na kuacha utaratibu huo unaonekana kuwa na mzunguko mrefu.

"Miye nashangaa mwizi amekamatwa katika wilaya yetu badala ya kufikishwa katika vituo vyetu vya polisi na kufunguliwa mashtaka anapelekwa jijini Mwanza kushtakiwa, inamaana hapa hawawezi kufungulia kesi na kuwajibishwa kisheria? Naomba tabia hii ishie kuanzia leo na tufanya kazi kwa kuzingatia sharia," alisema Mhita.

Aidha, aliwaagiza kuwapatia kipaumbele cha kazi zisizokuwa na elimu wananchi wanazunguka mradi huo ili wawe walinzi wa vifaa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mhita alitaja hatua za kudhibiti wizi katika mradi huo kuwa ni vyema wakashirikisha Jeshi la Jadi (Sungusungu) lililopo ndani ya jamii ambalo limekuwa likifanyakazi pia kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Meneja mradi wa SGR kipande hicho, Sun Sanguang, alisema asilimia kubwa ya ulinzi wa vifaa vya ujenzi wa mradi umekuwa ukifanywa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa kufanya doria maeneo yote na wamekuwa wakifanya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Alisema vitu ambavyo vimekuwa vikiibiwa mara kwa mara ni mafuta, nondo, saruji, pamoja na mbao na kwamba mafuta yamekuwa yakiibiwa hasa nyakati za asubuhi na mchana.

Alisema ili kuondoa wizi huo wamejenga utaratibu wa kupima mafuta kwenye magari yanaporejea kambini baada ya kazi na kuangalia kilometa.

Msimamizi wa Mazingira na Usalama, Grace Mola alisema, kwa sasa wameongeza umakini katika ukaguzi hasa wa magari ili kuhakikisha vifaa vya ujenzi haviibiwi na mradi unakamilika kwa wakati.



Ukurasa 12

TFC yaainisha inavyojitosa mapambano ya usambazaji mbolea hadi 'kieleweke'




Ukurasa 13

Onyo hili la TCRA lisiishie kwa mpotoshaji huyu anayetukwaza



Ukurasa 14

**MIAKA MIWILI YA SAMIA**

**Dk. Ngailo: TFRA tumeboreshwa kote kwa mbolea, viwanda hadi maabara**

BUFE

IJUMAA MACHI 24, 2023

Nipashe

# Rais azindua kilimo biashara, wadau teknolojia wabuni yao 'kumsapoti'

## • Simu yaunganishwa na shughuli shambani

**Na Frank Monyo**

WIKI hii Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alizindua mradi wa mashamba makubwa maarifu 'block farming' ambayo ni maalumu kwa vijana wa kiume na wanawake (BBT) na kukabidhi mitambo ya umwagiliaji kwa tume ya Taifa ya umwagiliaji.

Wakati wa uzinduzi huo, alipata nafasi ya kuzungumza na wakulima wa Mradi wa Umwagiliaji wa Msagali. Mpwapwa na kisha wakulima wa Mradi wa Umwagiliaji wa Membe, Chamwino, Dodoma.

Anasema uzinduzi wa mashamba hayo makubwa, ni mwendelezo wa jitihada za serikali katika kuimarisha upatikanaji ajira kwa vijana na wanawake kupitia programu ya 'Jenga Kesho Iliyo Bora' (Building a Better Tomorrow - BBT).

Rais anaongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Kilimo imejidhatiti kuhakikisha mpango unakuwa endelevu na wa mafanikio yaliyokusudiwa. Miongoni mwa malengo ni kilimo, uvuvi na ufugaji, kuchangia asilimia 10 ya pato la taifa ifikapo mwaka 2030, kutoka asilimia 3.6 ya hivi sasa.

Ni hali inayodumisha taswira kwamba kilimo ni shughuli kubwa kiuchumi inayotegemewa na takribani robo tatu ya Watanzania wote, huku ikichangia karibuni asilimia 30 ya pato la ndani ya nchi.

Kimsingi, ni mwendelezo wa juhudi na itikadi tangu kupatikana uhuru wa nchi 'Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa' uliohimizwa na Mwalimu Julius Nyerere na haujawahi kuachwa katika awamu zote a uongozi zilizopita, kila moja kiwa na na mikakati yake.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. akimkabidhi mfano wa funguo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa. kwa ajili ya Programu ya Kilimo cha Mashamba Makubwa ya pamoja, Chinangali Mkoani Dodoma, tarehe 20 mwezi huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Inafahamika, kuna nyenzo za kudumu katika kilimo kitaofa, mathalan taasisi za tafiti wa kilimo zilizotapakaa kote nchini (TARI), mathalan Ilonga Morogoro; Ukiliguru Mwanza; na Uyole Mbeya, vyote vikibuni mengi kama mbegu bora na kinga ya magonjwa kilimo.

Katika zama zilikoko, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amefanya mapinduzi katika sekta hiyo, ikiwamo, bajeti yake kuongezwa maradufu katika mwaka uliopo wa fedha.

Ni mkakatio uliozama katika kilimo cha kisasa, umwgiliaji na teknolojia, sura ya biashara na kusaidia vijana, ruzuku ya mbolea, hali kadhalika ulingo wa uwekezaji kitaifa, ikilenga ichangie asilimia 10 pato la taifa.

Baada ya kuzindua Mradi wa Kilimo kwa Vijana huko Mpwapwa Dodoma wiki hii, Rais Dk. Samia akapokea salamu za pongezi kutoka ulingo wa vyama vya siasa vya upinzani, kwamba kinafanyika kile wanachokililia miaka yote, ikiwa katika sura aliyoiomba wakati 'anavifungulia' kushiriki mkitasanyiko ya kiasiasa, kwamba "wamkosoe kistaarabu anapokosea na anapopatia apewe pongezi."

**WATAALAMU WAUNGANA**

Mbali na kuungwa mkono ki siasa, pia taasisi za kitaalamu zimeguswa kumuunga mkono kwa vitendo vya kitaalamu.

Kuna taasisi tofauti zimejitokeza kuwekeza kuleta majibu ya malengo, kupitia ubunifu wa kiteknolojia kusaidia kilimo na wakulima kwa ujumla nchini, mojawapo ni kampuni ya Vodacom Tanzania.

Hao wamewekeza kwenye kuwatafutia majibu wakulima, kupitia huduma ya kidigitali ya 'M-Kulima', mfumo unaowaunganisha wadau wote wa sekta ya kilimo, kurahisisha mawasiliano na kufanya miamala baina ya kampuni, serikali au mkulima muda wowote.

Ni huduma inayotajwa kufanya kazi kukusanya taarifa zote muhimu kama vile eneo la makazi, ukubwa wa shamba na mazao, zikiwa taarifa muhimu, kwani zinatumika kutoa ushauri kuhusu mazao na hali ya hewa.

Hapo inamaanishaa, mkulima anaweza kuufikia mfumo huo na kupata taarifa kuhusu mazao bora ya kilimo kwa wakati uliopo, kulima, wadudu na kuvuna, ukitoa nafasi kwa mkulima, baada ya kuvuna, mazao huchukuliwa na kupelekwa ghalani.

Inalelezwa katiam hatua hiyo, anapewa taarifa za kuhifadhiwa kidigitali na mkulima anapatiwa uthibitisho, kupitia ujumbe kwenye simu yake ya mkononi na baada ya hapo, mkulima hupokea malipo ya mazao yake kwa simu mkononi.

Mwezi huu, Vodacom kwa kushirikiana na kampuni Smart Lab waliendesha ushindani wa programu iitwayo 'Digital Accelerator'; kampuni 12 chipukizi za kiteknolojia zilifanya maonyesho na uwasilishaji mbele ya jopo la majaji wa ndani na kimataifa.

Ni maudhui yaliyohusu bidhaa zitakazotoa majibu na suluhisho la ubunifu wa kiteknolojia kwa changamoto tofauti zinazoikabili jamii ya Watanzania.

Kampuni tatu zilitangazwa washindi; wa kwanza Bizy Tech kupitia huduma yake ya Kilimo BaNDO, wakati Smart Darasa na Twenzao wao walishika nafasi za pili na tatu. kila mmoja

**INAENDELEA UK.14**

BIASHARA

# TFC yaainisha inavyojitosa mapambano ya usambazaji mbolea hadi 'kieleweke'

**Na Beatrice Moses**

HADI sasa hatua za kufikisha mbolea kunakotakiwa kwa wakulima na bei sahihi, haijakaa sawa na hasa kwa mazao ya biashara.

Mhusika, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), inasema imeshaliona, hivyo na kuchukua hatua za usahihi kufikisha mbolea ya ruzuku kunakostahili na kwa malengo sahihi.

Meneja Mkuu wa TFC, Samuel Mshote, anabainisha baadhi ya changamoto zilizopo, zinajumuisha kukosekana mtaji wa kutosha.

Anaainisha hali, TFC inahitaji fedha shilingi bilioni 45 kukidhi huduma za usambazaji mbolea kwa wakulima nchini kote, akiahidi kwamba pindi zitakapopatikana, watazitumia kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi, hatua itakayowezesha kuwapo mbolea nyingi nchini, hata ikapatikana kirahisi na kutimiza mahitaji ya kilimo msimu wa sasa.

Inaelezwa kwamba, hatua ya kusambazwa mbolea inayozalishwa na viwanda vya ndani, inategemea kuwapo fedha za kutosha za kuagiza moja kwa moja bidhaa hiyo kwa njia ya usafiri wa ndege, kufanya mbolea ikapatikana kwa wingi na bei itakuwa chini kwa wakulima, hata kupanua kilimo chenye tija kitaifa.




Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kushoto), akishiriki kwenye ugawaji mbolea ya ruzuku. **PICHA: MTANDAO.**

Hapo anafafanua hatua iliyoko, ni kwamba TFC inasambaza mbolea ya ruzuku tangu Januari 28 mwaka huu, ikiaminika inawaletea ahuweni wakulima.

"Ni mbolea ya kukuzia, hii ni ya ruzuku, imetengenezwa na viwanda vya hapa nchini, tunaanza kuisambaza kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini," anasema.

Mshote anasema, TFC inatambua mahitaji ya mbolea nchini hadi mwezi uliopita ilikuwa tani 430,000 wakati ya ruzuku ni tani 2700 na kwa kuanzia wakati huo magari saba yenye tani 210 yalianza safari siku hiyo Januari 28 kuelekea mkoani Rukwa.

Anaeleza mbolea ya ruzuku kwa mkulima anayoipata shilingi 70,000 (asilimia 62 ya bei halisi) kwa ujazo wa kilo 50, wakati kwenye soko inauzwa shilingi 112,000, wamekusudia kuhakikisha inafika kwa wakati kwenye maeneo yote yaliyolengwa.

Kwa mujibu wa Mshote, sasa TFC ipo kwenye mchakato wa kuhakikisha uzalishaji mbolea nchini unaanza na katika maandalizi, eneo la kujenga kiwanda limepatikana wilayani Kisarawe.

Anasema, wameshafufua mazungumzo ya awali na wawekezaji kutoka nchini Morocco, hivyo wanaamini ni hatua itakayofanikiwa.

Mkurugenzi wa TFC, anasema hadi sasa wanakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwamo mtaji mdogo, upungufu wa rasilimali watu, miundombinu chakavu na kukosa vitendea kazi, ikiwamo magari ya kusafirisha mbolea.

Mkurugenzi wa Bodi ya TFC Dk. Frolence Turuka, anataja wajibu wa kampuni hiyo, kujipanga kuhakikisha inaanza kuzalisha mbolea na kuwezesha upatikanaji wake kwa uhakika nchini, pia kutimiza mipango ijayo, ikiwamo kuzalisha kwa wingi na kuuza nje.

NAIBU WAZIRI

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, anafafaua kuwa serikali imeshaipatia TFC shilingi bilioni sita mwaka huu, ili kuiwezesha kutekeleza baadhi ya mipango yake iliyojiwekea.

Mavunde anataja eneo mojawapo, ni kufanikisha lengo la kukuza kilimo kutoka asilimia 3.6 ya sasa na kufikia asilimia 10 mwaka 2030.

"Katika kuhakikisha kuwa lengo lililowekwa linafikiwa serikali imenunua pikipiki kwa ajili ya maofisa ugani, ili kuwawezesha kutoa huduma katika maeneo yaliyopangwa. Pikipiki hizo zimefungwa vifaa maalum vya kubaini eneo husika alilopangiwa," anasema.

Anasema, pia ugawaji mbolea unapaswa kuzingatiwa na aina ya udongo iliyopo katika sehemu husika, ili kupatikane tija, hivyo maofisa ugani wanapaswa kutimiza majukumu yao kuhakikisha wanatoa ushauri bora wa matumizi ya mbolea na upandaji mbegu.

Naibu Waziri anasema, serikali inatambua kuwapo changamoto kwenye ugawaji wa mbolea ya ruzuku inazitatua, pia itahakikisha msimu ujao wakulima wanapata pembejeo kwa wakati.

"Tumekusudia kuhakikisha vituo vipya vya mawakala wa kusambaza mbolea za ruzuku vinasajiliwa, pia na vyama vya ushirika vitatumika vyema katika kuhakikisha inapatikana kwa wakati," anasema.

WADAU WA KARIBU

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Miko Zenzera, wa Mbozi mkoani Songwe, Sara Nzunda, anasema hatua ya serikali kufuatilia kwa karibu usambazaji mbolea ya ruzuku, ni njema kwa kuwa inasaidia kuwafikia wakulima kwa uhakika wa bei iliyopangwa.

Anarejea mwaka jana, baadhi ya wakulima waliangukia wakati mgumu, kwa baadhi ya wakala mbolea zikafika mikononi mwa walanguzi, hata wanashindwa kupata mbolea kwa bei iliyopangwa ya shilingi 70,000 wakijitetea kwa visingizio vingi,

"Tumepata shida miezi kadhaa iliyopita, unaiona mbolea dukani na mkononi una shilingi elfu 70, lakini ajabu unaambiwa mbolea imelipiwa, baadaye baadhi ya watu wakadai kwamba watu wanaokwenda na shilingi elfu 85 wanapewa mbolea," anasema.

Nzunda anasema, kwa sasa mbolea hiyo inapatikana kwa uhakika na kwa bei inayotangazwa serikalini, hivyo anaishukuru serikali kwa usimamizi makini, hatua inayowapa wakulima moyo kuendelea kulima mazao mbalimbali, yakiwamo ya biashara.

# DC mstaafu Betty Mkwasa katika maisha uwekezaji, sasa atwaa tuzo ya kampuni bora

## • Asimulia mapito mapya hadi mafanikio

**Na Elizabeth Zaya**

ANAITWA Elizabeth Mkwasa (pichani), Mkuu wa wilaya zamani wa Bahi na Mvomero, ambaye mzizi wake ni uanahabari akipata uteuzi huo akiwa kwenye kipaza sauti cha IPP. Leo hii ni mfanyabiashara anayetunukiwa tuzo, mshindi kwenye tuzo za viwanda kwa wanawake wajasiriamali Tanzania.

Hiyo ni katika kategoria ya matangazo na uchapishaji, kuwawezesha wanawake katika eneo hilo, zilizotolewa hivi karibuni na Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), katika tuzo zitolewazo kila mwaka kumpata mwanamke bora.

Betty, mmiliki wa kampuni ya matangazo na uchapishaji ya BB BOND, anaeleza kwamba tuzo hiyo imemwongezea nguvu ya kufanya kazi zaidi.

"Mimi nilishinda katika kategoria ya 'branding and Printing' na nilishika nafasi ya kwanza, jambo hili limenitia moyo na namshukuru Mwenyezi Mungu," anasema Mkwasa.

"Nimejifunza mengi sana kutoka TWCC katika utoaji wa tuzo hizi kwa sababu wanazingatia sana ubora pamoja na jinsi ulivyowawezesha wafanyakazi wako au wanawake katika kampuni yako.

"Wanaangalia pia utofauti kati yako na wafanyabiashara wenzio, muda ulioendesha kampuni, kama ni ya kwako binafsi au unashirikiana na wenzio na kwa kiwango gani."

Anafafanua siri ya mafanikio yake kwamba: "Unajua haya mambo ya kuweka mabango makubwa barabarani, kuchapisha tisheti, wengi tunaona wanafanya wanaume.

"Mimi nina wasichana waliokuwa wanafanya shughuli za usafi na nyingine ndogo ndogo katika ofisi yangu, nikawapeleka wakajifunza na nikaona kwa nini tuwaajiri wengine wakati hawa tunaweza kuwaendeleza wenyewe.

"Tulichofanya tukawaendeleza kupata utaalamu wa namna ya kufanya hizo shughuli na sasa hivi hawafagii tena wala hawafanyi hizo shughuli ndogo, isipokuwa wamekuwa maalum kwa shughuli hizo za kutengeneza matangazo makubwa pamoja na shughuli zote za uchapishaji."



Anaeleza kadri siku zinavyosogea, ndivyo wasichana hao alivyowawezesha wanavyozidi kubobea kikazi na wanazipenda kuliko ilivyokuwa awali wakati kwenye uhudumu.

"Unajua kina dada kwenda kupanda na kupigilia hayo matangazo makubwa siyo kazi rahisi, anaweza akajisikia vibaya, lakini baadae walikuja kuipenda kazi yao hiyo na wanasafiri hadi mikoani," anasema Mkwasa.

### WOGA WA KINAMAMA

Betty anasema, tangu waingie katika biashara hiyo inayoogopwa na wanawake wengi ya kuweka mabango makubwa na uchapishaji, maisha yao kiuchumi yamebadilika kwa kiwango tofauti na ilivyokuwa awali.

"Sasa wanazungumza lugha nyingine kabisa, ukiwakumbusha awali kabla hawajaingia katika biashara hii wanacheka sana, wanaishia kusema tunakushukuru kwa kweli kwa kutoa kule, maana hali zetu mpaka sasa zingekuwa hazieleweki.

"Tuliwachukua mahali ambako nako huko walikuwa wanafanya kazi ya usafi, tukawaleta kwetu nako wakawa wanafagia. Kwa hiyo kwa sasa wanashukuru," anafafanua Betty na kuendelea:

"Kwa hiyo mimi nasikia faraja sana kuona wana furaha na kazi hii na ni moja ya mambo ambayo nafurahia ninapomkwamua mwanamke mwingine kiuchumi."

### VUTA NIKUVUTE

Betty anasema, matangazo na uchapishaji, shughuli zake zinajihusisha kuomba tenda, ambayo nayo inahitaji tenda zaidi kuzifanikisha mbayo si kazi ndogo. Anasimulia kinyang`anyiro hicho, asilimia kubwa washindani wao ni wanaume, lakini yeye amekuwa akijitosa kupambana, katika hali inayohitaji uvumilivu.

"Nimeona kazi hii ya 'branding' ina faida, japo ni ngumu sana, yaani ni lazima upambane sana. Pia soko lake ni gumu, linalohitaji upambane na ukitaka kazi kubwa katika eneo hili la branding, ni lazima uingie kwenye tenda, iwe kwenye benki, serikalini na kwingineko.

"Kwenye tenda ndiko kwenye mapambano makubwa sana, unakutana na watu wenye fedha nyingi na kibaya zaidi kinachofanya iwe ngumu ni wale watu wa kati.

"Yaani unakuta mtu hana mashine, hana chochote lakini anaingia kwenye tenda, isipokuwa wao wanakuwa na fedha. Wanakuwa wanasubiri ufanye kazi wewe halafu wao wametulia kusubiri fedha yao," anasema.

### USHAURI WAKE

Anashauri, ni vema tenda zinazotolewa kwa waombaji ziende sambamba na kukagua ofisi zao, kabla ya kuwapatia hizo kazi za tenda.

"Ili na sisi tupate, ambao tuna mashine zimekaa tu zinaoza, watoa tenda wawe wanakuja kukagua, kabla ya kutoa tenda kwa mtu.Tunaomba wote tukaguliwe kama tuna mashine, la sivyo tutaendelea kuumia kila siku.

"Ukaguzi ndio utakuwa suluhisho la hili kwa sababu utakuwa unaangalia uhalisia wa kampuni wanayoipatia hiyo tenda. Kwa mfano mimi nikiomba, mtu mwingine naye akiomba, kila mmoja apitiwe akaguliwe kujihakikishia..."

### SALAMU KWA TWCC

Sasa anakishukuru Chama Cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), kwa uwezeshaji endelevu wa kinamama kiuchumi.

Anasema: "Nilipoingia kwenye hicho chama, nimefanya mambo mengi sana na nimesafiri nchi nyingi kwa ajili ya chama hiki, wanatupatia mafunzo na mara nyingi wanatuitia na watu wa benki kutuelimisha jinsi gani ya kukopa..."

Rai yake ni kwamba wanawake wengi wanaogopa kuthubutu, hasa penye changamoto. Anaendelea: "Hata nilipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi, katika halmashauri kulikuwa na mikopo ile ya asilimia 10, inayokwenda kwa vijana na wanawake.

"Tuliona kwamba wanawake walikuwa wanarejesha haraka kuliko vijana, kwa sababu ya nidhamu fulani walio nayo. Sasa hiyo ndio inawapelekea wanashindwa kujaribu na vitu vingine, wanaona kwamba huenda wakifanya hiki na kile watakwama na wakikwama itakuwaje?"


Betty anataja jambo jingine, ni kwamba wanawake wanaogopa hasara, hata kuchangia nayo washindwe kuthubutu na kutokata tamaa ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu.

"Ukifanya kimoja kikadunda, fanya kitu kingine. Mimi namkumbuka hayati Reginald Mengi (Mwenyekiti wa Kampuni ya IPP), alikuwa anafanya biashara ya vitu vingi vingi, kwa hiyo ile kujaribu ni muhimu sana mpaka ufike mahali panapokuinua."

"Mfano nilivyoanza kuwaingiza hawa wasichana kwenye hii kazi, sikuwaambia moja kwa moja, nilianza kwa kuwaambia watafute wateja halafu wanapata sehemu ya malipo yao.

"Mwisho wa siku nikaona wanafaa kwenye biashara nikawaendeleza na mpaka sasa wanashukuru sana, japo mwanzoni waliona ni ngumu. Hiyo ndiyo hulka ya wanawake kuogopa," anahitimisha.

TAFAKURI YA MLALAHOI




# Onyo hili la TCRA lisiishie kwa mpotoshaji huyu anayetukwaza



**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**(kulangwasos@gmail.com)**

NI kweli kwamba angalau katika miaka hii miwili ya Chifu Hangaya, Tanzania katika tasnia ya habari kuna kijiuhuru hivi! Tunaandika, tunatangaza bila kutishwatishwa au kuitwaitwa.

Tunafanya hivyo, bila hata kufungwafungwa. Mazingira hayo yamewekwa na Rais wa Sita, Dk Samia Suluhu Hassan a.k.a Chifu Hangaya, kwa anachoamini katika uhuru wa kujieleza, uhuru wa kutoa na kupata habari.

Chifu Hangaya ndiye aliyeamua vyombo vya habari vikiwamo vijitivii vilivyokuwa kifungoni, kuachwa bila masharti na viendelee kufanya kazi zao kama kawaida, lakini vikijichunga katika kufuata sheria.

Hata hivyo,tunaonekana nasi kujisahau na kudhani kuwa ukishapewa uhuru, basi hutafuatiliwa tena na kujikuta tukifanya mambo mengine ambayo hata hayana msingi. Tukifuatilia mengine na kuyarusha huku tukijua hayana mashiko kwa jamii.

Angalia hivi karibuni, kaibuka binti mmoja hivi mbele ya tivii moja, akihanikiza kuwa alikuwa ziarani mbinguni alikokutana na Mungu na kushuhudia maghorofa yaliyojengwa huko yakiwa marefu na ya dhahabu tupu.

Nasi bila kutambua, bila kujua tunafanya nini, tukampa muda kwenye vijitivii kuuhadaa umma tena wa dunia nzima, kwamba ni mtu wa kwanza kuonana na Mungu na kukaa naye meza moja, sijui alikula naye nini?

Wapo walioshabikia video ile, lakini wengi bila shaka waliiponda na kuhisi pengine kuna tatizo la afya ya akili kwa anayesimulia mambo ambayo hayawezekani kabisa. Sina uhakika kama alieleza alitumia usafiri gani kufika mbinguni!

Kwa wale tuliokereka na mahojiano hayo, tunaiunga mkono Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa onyo ililotoa kwa vyombo vya habari, kuhusu kurusha maudhui kama hayo kwa jamii ambayo kwa kweli hayana staha.

Hayana staha kwa sababu yanaingilia imani za kidini, kweli tuaminishwe kuwa fulani anaweza kwenda Mbinguni akakutana na Mungu na kukaa naye meza moja jamani? Wakristo na Waislamu tunaamini Mungu mmoja, hii si kashfa kwetu?

Hivi kwa kujiita nanihii ndipo atupande vichwani na imani zetu na sisi kumpa wasaa wa kuidanganya Dunia? Tunawashukuru TCRA kwa kuingilia kati na kuonya, ili wasiibuke mitume wengine bandia kama hawa wakapewa fursa ya kutuvuruga.

Kwa kuwa TCRA wamekemea dhidi ya mawazo haya fikirika yanayogusa imani za kidini, sisi wenye vyombo hivi vinavyosambaza habari na taarifa haraka kwa jamii, tujiangalie tusikaribishe watu tusiowajua kiimani na kiakili na kuwapa fursa ya kututukanisha na Mungu.

Hilo lisiishie hapo, bali pia majumba ya ibada ambayo hivi sasa yanaibuka kama uyoga nchini yafuatiliwe, kwani nayo yanamiliki vijitivii vya aina hiyo na kurusha mawazo fikirika yakiwamo ya uponyaji ambao ni bandia.

Tuna makanisa-si misikiti, yanayohubiri uponyaji, huku mengine viongozi wao wakijiita maaskofu, wakijimwambafai kufufua wafu na kuendelea kuwapora waumini wao fedha, kwa kinachoitwa sadaka, huku wakiwauzia pia maji, mafuta na chumvi kwa bei mbaya.

Kwa upungufu wa uelewa wa baadhi yetu, tumekuwa tukipoteza raslimali zetu na hata maisha kwenye majumba hayo kwa imani za kuongoka na kuponywa, lakini tukiendelea kubaki na matatizo yetu bila unafuu wowote, huku maaskofu hao wakitegeshea walemavu bandia na kudai kuwaponya.

Tanzania tunaweza kujifunza kwa mataifa mengine ambayo zamani yalikuwa nyuma na leo yako mbele na kuyatumia kama mifano, hasa linapokuja suala la kusimamia jamii. Kuna mataifa jirani tu yanaonekana kutuongoza hivi sasa, kwa mambo mengi na kulazimika kujifunza kwao!

Nakumbuka miaka mitano iliyopita, nchi jirani ilifunga nyumba za ibada idadi ya mamia katika mji mkuu wao, kwa walioshindwa kufuata masharti ya usafi na usalama, tunashindwa nini kufuatilia pale tunagundua au kuthibitisha upotoshaji wa aina yoyote?

Tuhakikishe tunaepukana na mawazo hayo ya kuonana na Mungu, au mengine yasiyo na uhakika au yenye mwelekeo wa kupotosha. Wanahabari nasi kabla ya kurusha mambo haya, ni vema kuchungulia nyuma ya pazia kuna nini na kuwa na uhakika. Tusipotoshwe na wapotoshaji hawa. Alamsiki!

UCHUMI

## MIAKA MIWILI YA SAMIA

# Dk. Ngailo: TFRA tumeboreshwa kote kwa mbolea, viwanda hadi maabara

**Na Renatha Msungu, DODOMA**



Waendesha pikipiki, wakiwa wamebeba mbolea ya ruzuku za wakulima. **PICHA: MTANDAO.**

Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan alizindua mpango wa ruzuku ya mbolea mnamo Agosti 8 kwenye Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima, yaliyofanyika katika viwanja vya Mwakangale, jijini Mbeya.

Hapo akaitaka Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuanza utekelezaji wa mpango huo mnamo Agosti 15, 2022.

Hadi sasa, mbolea imeshatawanywa takribani mikoa yote nchini na kutoa nafasi kwa wakulima kuipata kirahisi, hiyo ikimaanisna ni kitendo hicho kimewaibua wakulima na kilimo nchini, kulingana na sehemu anayoishi.

Nipashe imezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, anayesema mzizi unaanzia na kupanda bei ya mbolea kwenye soko la dunia, hata wakulima wengi kutoweza kumudu gharama zake. Serikali ilitenga Sh. bilioni 150 kugharamia ruzuku kwa msimu wa kilimo 2022/2023.

Anasema kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 gharama za mbolea zilipanda ghafla na wakulima walinunua bidhaa hiyo kwa bei kuanzia Sh. 100,000 hadi 150,000 kulingana na umbali anakonunua.

Dk. Ngailo anaeleza utoaji ruzuku umezingatia mahitaji halisi ya mkulima nchini, kulingana na taarifa za usajili na bajeti ya serikali na kubainisha kuwa mbolea zilizohusika katika Mpango wa Serikali wa Utoaji Ruzuku na zile za kupandia, zikiwa ni nusu ya matumizi yote ya mbolea nchini ;mbolea za kupandia na kukuzia za aina nyingine nazo zimehusishwa , kulingana na mahitaji ya soko.

Katika kuhamasisha matumizi ya mbolea za nchini, mbolea nazo zimeingizwa kwenye mpango wa ruzuku, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Dk. Ngailo anaeleza mfumo huo umetumia programu maalum kidijitali kuratibu utekelezaji, kuanzia utambuzi wa washiriki wa mfumo wakiwamo waingizaji na wazalishaji wake, wafanyabiashara na wakulima zitakazoratibu usambazaji; uuzaji mbolea kwa wakulima; na malipo ya ruzuku ya mbolea.

Anasema hadi kufikia mwezi uliopita, waingizaji wa mbolea 28 wamesajiliwa, wazalishaji watatu, wakala na wasambazaji mbolea 3,303 wanaotumika katika mikoa yote 26 nchini.

Pia, anaeleza kuwa hadi tarehe hiyo, kushirikiana na serikali za mitaa, imeshasajili wakulima 3,264,440 wenye vigezo vya kunufaika na mbolea za ruzuku.

**HALI YA VIWANDA**

Hali ya kuongezeka viwanda vya kutengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea, Dk. Ngailo anasema kuna jumla ya viwanda 16 vya kuzalisha mbolea na visaidizi vyake (chokaa na gypsum) ,ambavyo ni vitatu vilivyoko mikoa ya Dodoma na Tanga, akiainisha, vipo viwanda 10 vya kutengeneza mbolea za maji na sita, hutengeneza mbolea za punje.

Dk. Ngailo anamsifu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhamasisha wawekezaji binafsi nchini, akitaja mfano wa kutoka nchini Burundi, yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa kiwanda, jijini Dodoma na kimeshaanza uzalishaji tani 200,000 kwa mwaka, lakini kitakapokamilika, kitazalisha tani milioni moja na tani 300,000 za chokaa.

**WAPATA MAABARA**

Anasema, itapunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje, huku ujenzi wa maabara kupima mbolea ya TFRA ukiendelea, kwani imekuwa ikitumia maabara za taasisi nyingine kupima ubora wa mbolea, hali inayochangia ucheleweshaji wa kupata majibu, hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya udhibiti.

Anasifu ndani ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mamlaka yao ilitengewa bajeti kuanza ujenzi wa maabara ya mbolea na hadi mwezi uliopita, ilifikia asilimia 95 na kwamba itawaongezea ufanisi katika kazi yao.

Kwa mujibu wa Dk. Ngailo, maabara hiyo inatarajiwa kutumiwa na nchi jirani za Malawi, Zambia, DRC, Burundi na Rwanda, hivyo kuongezea nchi mapato.

**UPATIKANAJI MBOLEA**

Kuhusu hali ya upatikanaji mbolea nchini katika miaka miwili iliyopita, Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Joseph Charos, anasema kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikuwa tani 546,818 na matumizi tani 475,870.

Anafafanua, hadi kufikia Januari mwaka huu, upatikanaji wa mbolea nchini umeongezeka kufikia tani 678,528 sawa na asilimia 102 ya mahitaji nchini, matumizi yakikadiriwa ni tani 667,730 ifikapo mwezi Juni mwaka huu, msimu wa kilimo unapofika mwisho.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Happines Mbele anasema, mifumo ya udhibiti wa mbolea nchini imeendelea kuimarishwa na kuhakikisha inawafikia wakulima kwa ubora, bei nafuu na kwa wakati.

Anasema udhibiti tajwa umewezekana kutokana na kuongezeka idadi ya wakaguzi wa mbolea nchini, kusajili wafanyabiashara wa mafunzo ya kila mara kwa mfumo wa uendeshaji wa biashara ya mbolea.

Happiness anataja mgawanyo wao; kuanzia mwaka 2012 mpaka sasa kuna wakaguzi wa mbolea 140 katika Ofisi za Mamlaka na Halmashauri za Wilaya; na maofisa kilimo 59 kati ya 140 waliopata mafunzo ya ukaguzi, wakisubiri kutangazwa kwenye gazeti la serikali, ili waendelee na jukumu la kudhibiti ubora wa mbolea.

Mkurugenzi huyo anasema, hadi sasa idadi ya wafanyabiashara wa mbolea imeongezeka kutoka 1,691 mwaka 2020/2021 hadi 4,776 mwezi uliopita, akijinasibu ni mafanikio makubwa.

Anaeleza matumizi ya mbolea nayo sasa yako juu maradufu, Happiness akisema yameongezeka kutoka tani 426,550.41 mwaka 2021/ 2022 hadi zaidi ya tani 667,730 kwa msimu huu wa kilimo.

Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi , Victoria Elangwa anaeleza kwa miaka miwili sasa, Mamlaka ilikuwa na ofisi moja tu ambayo ndiyo makao makuu jijini Dar es-Salaam, sasa imefanikiwa kufungua ofisi tano za Kanda, akizitaja: Nyanda za Juu Kusini (Mbeya); Mashariki (Dar Es Salaam); Kati (Tabora); Kaskazini (Arusha), na Ziwa (Mwanza).

**KAZI KWA TEHAMA**

Hapo anaungwa mkono na Meneja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Robert Mtendamema, anayeeleza kufanikiwa kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma kwa wadau wake, uitwao Mfumo wa Kimtandao wa Mbolea(FIS).

Anaeleza ni mfumo huo unaohudumia wadau, ikijumuisha wanaohitaji kujisajili kwa biashara ya mbolea, kusajili mbolea mpya, waingizaji wapya wa mbolea na wale wanaowasilisha maombi ya vibali vya kutoa na kuingiza mbolea nchini.

Anasema awali huduma zote zilitolewa kwa mfumo wa kawaida, unaotumia muda mrefu, ikihusisha kusafiri ili kukamilisha mahitaji ya wadau. Anataja iliyopo sasa ni sehemu ya ajenda kitaifa 'Kilimo ni Biashara'.

# RAIS AZINDUA KILIMO BIASHARA, WADAU TEKNOLOJIA WABUNI YAO 'KUMSAPOTI'

**INATOKA UK.11**

kupitia huduma zao za elimu na usafiri.

Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa kampuni ya Bizy Tech, Isabella Fernandes, anasema lengo la huduma yake ya 'Kilimo BaNDO' ni kutoa suluhisho la ubunifu wa kiteknolojia kwa changamoto za wakulima wadogo, wafanyabiashara wadogo na kati, pia wadau wengine wa kilimo, kuzifikia huduma rasmi za kifedha na kuboresha vipato vyao kupitia mifumo thabiti ya masoko.

"Nimefurahi sana kuwa mshindi wa kwanza wa programu ya 'Vodacom Digital Accelerator', kwani itakuwa msaada mkubwa kwenye kuboresha ufanisi wa kampuni na kuwafikia Watanzania wengi zaidi nchini kote.

"Inawaunganisha wakulima kwa urahisi na wigo mpana wa huduma zikiwemo kufikia mafunzo na ushauri kutoka kwa wataalamu wa kilimo kuhusu mbinu bora wakati wa kulima na baada ya kuvuna.

"Mafunzo haya huwasaidia wakulima kuzalisha mazao bora yanayokidhi vigezo vya soko, kupunguza hasara baada ya mavuno, na kuongeza mapato," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, ni huduma yenye dhamana ya mikopo kwa taasisi za kifedha zinazowakopesha wafanyabiashara wadogo na kati, huku ikiwapatia wao na wanunuzi wengine soko la uhakika kwa vyanzo vya mazao ya kilimo.

Ferbades anasema, tangu kuzinduliwa asasi yake mwaka 2020, 'Kilimo BaNDO' imeshasaajili wakulima wadogo zaidi ya milioni 2.87 na kuwasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati zaidi ya 129,035 kwenye kilimo cha mazao tofauti, kama vile mahindi, soya beans, korosho, alizeti, mihogo, mpunga.

Inayajwa kiwa inaongeza thamani katika kilimo cha mboga na matunda, huduma hiyo ikitengeneza mfumo wa mnyororo wa thamani unaowaunganisha wadau kutoka shambani hadi majumbani, akiwaoridgesha kuwa ni; wazalishaji pembejeo, wanunuzi wa mazao, na watoa huduma za kifedha.

**BOSI VODACOM**

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya simu Vodacom Tanzania PLC, Philip Besiimire, anasema: "Jambo la kipekee ambalo limenifurahisha, ni kuona mwanamke ameibuka mshindi. Bado waanzilishi na washirika wa kampuni hizi wengi wao ni wanaume.

"Nitumie fursa hii kutoa wito kwa serikali na wadau kuangalia uwezekano wa kuwa na programu ya aina hii mahususi kwa wanawake. Hii itachochea kuwa na wanawake wengi waanzilishi, pia itaongeza fursa kwa wanawake nao kuwapo kwenye nafasi za juu kwenye mfumo wa uongozi kwenye kampuni hizi.

"Kwa kuongezea, kuwapo pia na majukwaa maalum kwa walemavu ili kuonyesha uwezo ili kuongeza ujumuishi kwenye ngazi zote za jamii,"

Kampuni 12 zilizofika fainali ni Shule Yetu Innovations, Smart Darasa, Lango Academy, Vijana Tech, Hack it Consultancy, Seto, Twenzao, Get Value, Spidi Africa, Medpack, Bizy Tech, na Bizzy Pay.



# Makandarasi wazawa walia kucheleweshewa malipo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Makandarasi nchini, Thobias Kyando, amesema licha ya serikali kuwapa kazi nyingi za ujenzi makandarasi wazawa lakini tatizo la ucheleweshaji wa malipo bado ni kero.

Alibainisha hayo jana jijini hapo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuundwa kwa Umoja wa Makandarasi, Wauzaji, Wasambazaji na Wakodishaji wa Mitando ya Ujenzi (TUCASA).

Alisema lengo la kuundwa kwa umoja huo ni kuwa na nguvu ya pamoja ambayo itawasaidia kutatua kero mbalimbali zinazowakabili katika sekta hiyo nchini.

Kyando alisema uwepo wa vyama vingi vya makandarasi kumesababisha kukosa nguvu ambayo wangeitumia kudai haki zao ambazo wamekuwa wakizilalamikia mara kwa mara.

Alisema moja kati ya kero ambazo bado makandarasi nchini wanakabiliana nazo ni ucheleweshwaji wa malipo baada ya kukamilisha kazi zao hali ambayo inawafanya wengi wao kuwa katika hali mbaya kiuchumi.

"Tumeona na tumekubaliana badala ya kuwa na vyama vingi vya makandarasi tuwe na umoja wetu ambao utajumuisha makundi yote kama vile makandarasi wanawake, makandarasi wazawa pamoja na wale wa nje ili tunapopaza sauti zetu ziwe na nguvu ya pamoja,"alisema.

Aidha alisema hivi sasa makandarasi wamekuwa wakilalamikia masuala mbalimbali ya kimaslahi lakini sauti zao zinaishia katika vyao.

Alisema: "Hivi sasa kama mkandarasi anatatizo basi inakuwa lake labda pamoja na chama chake, lakini kama tutaungana basi malalamiko yetu yanaweza kuwa na nguvu na kufika kule tunakohitaji.

Kyando aliongeza: "Tatizo lingine ni pale ambapo mkandarasi anachelewa kukamilisha mradi anatakiwa kuilipa fedha serikali lakini serikali inapochelewesha malipo hakuna wa kulizungumzia," alisema.

Kadhalika alisema kutokana na vita vya Russia na Ukraine vifaa vya ujenzi vilipanda bei wakati tayari makandarasi walishaingia mikataba ya ujenzi na serikali.

Alisema: "Na unapoingia mikataba na serikali wanadai iko fixed lakini vitu vimepanda bei kwa zaidi ya asilimia 40 haiwezekani mkataba ukabaki kuwa fixed, hivyo tunaimani kuwa kupitia umoja huu mambo kama haya tutakuwa na sauti ya pamoja na kuyasemea ili kuondoa mzigo wa hasara kwa makandarasi".

Hata hivyo alisema tayari maandalizi ya kuunda umoja huo yamekamilika na wanatarajia kufanya kikao jijini Dar es Saalam, ambacho kitakuwa na lengo la kupitia katiba na mambo mengine ili kuboresha baadhi ya vitu.



Ofisa Utekelezaji wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Kati, Emmanuel Ndejembi (kushoto) na Ofisa Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa Kanda hiyo, Prisca Matagi, wakikagua dawa na vifaa tiba zilizokamatwa kutokana na muda wake kuisha kabla ya kuteketezwa na moto kwenye tanuru lililopo Hospitali ya Benjamini Mkapa jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yajipanga kutokomeza TB ifikapo mwaka 2030

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na wadau katika sekta zote nchini ili kudhibiti na kuutokomeza ugonjwa wa kifua kikuu (TB) ifikapo mwaka 2030.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dk. Jim Yonazi, alisema hayo juzi katika kikao na makatibu wakuu wa wizara kilichofanyika jijini hapo.

Dk. Yonazi alisema ili kudhibiti ugonjwa huo ni muhimu kushirikiana na wadau wa sekta ya afya, elimu, usafirishaji pamoja na sekta nyingine ili ziweze kutoa michango yao.

"Tunahitaji kushirikiana na sekta mbalimbali kwenye hili la kupambana na ugonjwa wa kifua kikuu, lengo letu ifikapo mwaka 2030 tuwe tumeidhibiti na kuitokomeza TB," alisema Dk. Yonazi. Aidha, aliwataka wadau kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha anatoa mchango wake kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa TB na kuongeza kuwa jitihada za pamoja zitaleta matokeo chanya.

Mtaalamu Mshauri kutoka STP, Oscar Mukasa, wakati akiwasilisha taarifa ya mpango kazi wa kudhibiti ugonjwa huo alisema watu wenye hatari zaidi ya kupata ni pamoja na wale wanaoishi kwenye makazi duni, watoto, wavuvi na kwenye mabweni.

Mbali na hilo alisema watu wenye Virusi Vya Ukimwi (VVU), utapiamlo, wachimbaji madini, ambao wanaishi na mgonjwa wa kifua kikuu, watoa huduma za afya na wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano ni rahisi zaidi kupata ugonjwa huo. Kutokana na hilo alisema jamii inapaswa kuchukua tahadhari mapema ya kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu kwa kufuata taratibu za afya zinavyoelekeza.

Hata hivyo, aliwashauri wanaoishi katika mazingira hayo kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu ili kuwa salama.

# Bunge latoa tahadhari kwa h/shauri matumizi ya mil.500/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeitahadharisha Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuacha mvutano kuhusu matumizi ya Sh.milioni 500 zilizotolewa na serikali vinginevyo zinarudishwa serikalini.

Wabunge wa kamati hiyo wametoa tahadhari hiyo juzi baada ya kutembelea Hospitali ya Wilaya ya Manyoni na kuelezwa kuwa kumekuwa na mvutano kwa baadhi ya madiwani wakitaka fedha hizo zielekezwe kwenye ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Manyoni, Jumanne Mugalaza, aliwaeleza wabunge wa kamati hiyo kuwa madiwani wawili ndiyo wamekuwa wakileta mvutano kwamba zipelekwe kwenye ujenzi wa hospitali hiyo wakati maelekezo ya serikali ni kwamba zitumike kuboresha majengo ya Hospitali ya Wilaya.

"Mvutano huu ulikuwa na hoja ya watu wawili mbunge na Diwani wa Kata ya Manyoni ambao wanataka Hospitali ya Wilaya iliyopo sasa igeuzwe kuwa Kituo cha Afya na hivyo Sh. milioni 500 zianze kutumika kujenga hospitali mpya ya wilaya," alisema.

Kufuatia hali hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Denis Londo, alisema kama mvutano huo utaendelea kuna hatari ifikapo Juni 30, mwaka huu fedha hizo zinaweza kurudishwa hazina kabla hazijafanya kazi iliyokusudiwa.

"Kinachoendelea hapa hakijatufurahisha kama kamati na jambo hili halijengi taswira nzuri kwa wananchi kwani wanajua fedha zimeletwa kwa ajili ya kuboresha hospitali halafu kunakuwa na mvutano wa jinsi ya kuzitumia,"alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema fedha hizo zilizoletwa zinatumika kwa ajili ya kuboresha majengo ya hospitali na siyo vinginevyo na kuwahakikishia wabunge kwamba ifikapo Juni mwaka huu kazi itakuwa imekamilika.

Serukamba alisema fedha zinazoleta mvutano ni zile zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 023/2024, lakini zipo nyingine ambazo zilishaletwa na maboresho ya hospitali yanaendelea kama kawaida.





# NGOs zaombwa kutoa elimu kukemea vitendo vya ukatili

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Michael Semindu, ameyaomba mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kutoa elimu na kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia na mapenzi ya jinsia moja ambayo kwa sasa imekuwa tishio nchini.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao cha tathmni ya utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Shirika la RSCO linalofanya shughuli za usaidizi wa kisheria wilayani Mbarali.

Alisema kwa sasa ajenda kubwa ni kukabiliana na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja vinavyoendelea kushamiri duniani na kuyaomba mashirika kuisaidia serikali kukemea ili kuokoa kizazi cha sasa na baadaye.

"Kuna balaa na mapenzi ya jinsia moja, tumesikia na kuona kwenye vyombo vya habari kwa kweli hali ni mbaya, serikali inajitahidi kukabiliana na hali hiyo lakini peke yake haitoweza tunaomba mtusaidie kuongeza nguvu kwenye mapambano haya ili kuokoa kizazi chetu,"alisema Semindu.

Aliongeza kuwa Shirika la RSCO pamoja na kuisaidia serikali kupiga vita vitendo vya ushoga vilevile viendelee kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa kuzingatia miongozo na taratibu za nchi kusaidia haki kupatikana kwa wenye uhitaji.

Alisema msaada wa kisheria kwa jamii itasaidia kupunguza vitendo vya ukatili kama vile vipigo, ulawiti na ubakaji ambavyo vinaripotiwa kwenye jamii.

Aliahidi kutoa ushirikiano kwa Shirika la RSCO katika kutimiza majukumu yao ikiwamo kupatiwa ruzuku ambazo zinasaidia kufikia maeneo yaliyopo pembezo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la RSCO, Edison Mwakyembe, alisema kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2022 wanufaika 49,032 wamefikiwa na elimu ya kisheria kupitia elimu iliyotolewa kwenye jumuiya za kijamii, maadhimisho ya kitaifa na kimataifa, maadhimisho ya wiki ya msaada wa kisheria, vikundi vya kiuchumi vya kijamii pamoja na maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema elimu iliyotolewa inahusiana na ukatili wa kijinsia, ardhi, mirathi, ndoa, matunzo ya watoto, haki za watoto pamoja na madai mbalimbali.

Mwakyemba alisema kati ya mashauri 233 yaliyopokelewa kwa mwaka 2022 mashauri 123 yameisha na pande zote zimeafikiana. Mmoja wa wanufaika wa msaada wa kisheria, Angetrauda Mtega, alisema alikuwa mwathirika wa ukatili wa kiuchumi kwa mume wake kwa madai kuwa msimu wa kilimo walikuwa wanashirikiana, lakini ukifika wakati wa mavuno mumewe anahama nyumba na kuoa mwanamke mwingine.

Alisema hali hiyo imedumu kwa miaka 10 na kwamba alipopata elimu ya msaada wa kisheria mumewe alipewa elimu na alibadilika kwa sasa wanafanya kazi kwa kushirikiana na kupanga bajeti pamoja.



Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (aliyevaa miwani), akikabidhi mifuko 100 ya saruji kwa uongozi wa Shule ya Sekondari Kalobe jana, kwa ajili ya ujenzi wa choo kilichobomoka baada ya kuangukiwa na miti hivi karibuni. Pia alikabidhi Sh. milioni moja kwa ajili ya ujenzi huo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# CST yatoa msaada vifaa visaidizi kwa watoto 200

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SHIRIKA la kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum nchini (CST), imetoa msaada wa vifaa visaidizi kwa watoto 200 kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya.

Mkurugenzi wa Shirika la CST, Noela Msuya alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum.

Alivitaja vifaa visaidizi vilivyotolewa kuwa ni miwani, fimbo nyeupe, mafuta kwa watoto wenye ualbino kutoka mikoa mitatu ya mradi.

Alisema lengo kuu la mradi huo ni kuboresha maisha ya watoto wenye mahitaji maalum hasa wenye ualbino na wenye ulemavu wa kuona na kwamba Ubalozi wa Ujerumani iliwapatia Sh. milioni 226 kutekeleza mradi huo.

Alisema miongoni mwa mambo wanayojivunia kwenye utekelezaji wa mradi huo ni uhamasishaji wa kitaifa kwa Bunge la Tanzania kwenye masuala ya watoto wenye ulemavu sambamba na uhamasishaji wa haki, ulinzi na usalama wa watoto kwa mikoa nane nchini.

Katika kipindi cha miezi mitano ya utekelezaji wa mradi huo tumefanikiwa ushiriki wa ulinzi na usalama wa watoto kwa kuwafikia wazazi zaidi ya 50 na kufungua klabu za watoto kupigania 51 pamoja na walimu 600 kupatiwa mafunzo ya Elimu Jumuishi. Alisema tangu kuanzishwa kwa Shirika la CST miaka 15 iliyopita watoto wenye ulemavu wamenufaika kwa masuala mbalimbali ikiwamo kujengewa uwezo na maarifa ambayo yamewasaidia kujitegemea.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mradi huo, Damas Mwambije, alisema wanajivunia kuwa sehemu ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum ili waweze kutimiza ndoto zao kupitia elimu.

Hata hivyo aliuomba Ubalozi wa Ujerumani kufadhili tena mradi huo ili kuweza kukamilisha mambo ambayo bado hakuyafanya kwa kiwango walichokikusudia.

Akizungumzia faida za mradi huo, Mwalimu wa watu wasioona kutoka Shule ya Msingi Buigiri iliyopo mkoani Dodoma, Modest Ephraim, alisema elimu jumuishi imewasaidia kuwahudumia watoto wa aina zote kwa wakati mmoja.

Alisema elimu hiyo imesaidia kuwahudumia watoto wote bila kujali aina ya ulemavu walionao au kufundishwa kwa mbinu sawa ambazo zimewasaidia kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Aidha, alisema wamejifunza namna ya kuwalinda watoto wenye ulemavu, kuwafundisha namna ya kulinda ulinzi na usalama wao ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile ubakaji, ulawiti na vipigo.

# Jeshi la Polisi lapanda miti 428 kambi ya FFU

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya limepanda miti 428 katika maeneo ya makazi ya kambi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) mkoani Mbeya.

Hatua hiyo inaunga mkono jitihada za serikali kupanda miti ili kulinda vyanzo vya maji na kulinda mazingira.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Polisi ACP, Benjamini Kuzaga, jana aliongoza maofisa, wakaguzi na askari mbalimbali wa jeshi hilo kupanda miti kuzunguka mipaka ya kambi ya FFU.

"Katika zoezi hili jumla ya miche ya miti 428 imepandwa kuzunguka maeneo hayo lengo likiwa ni kuunga mkono juhudi za utunzaji na uhifadhi wa mazingira," alisema ACP Kuzaga.

Akizungumza baada ya zoezi hilo, Kamanda Kuzaga, aliwataka maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali kuendelea kuilinda na kuitunza miti hiyo ili ikue kwa ajili ya utunzaji na kupendezesha mazingira.

Aidha, alizishauri taasisi zingine kuiga mfano wao wa kupanda miti kuzunguka maeneo yao ili kuweka mazingira safi na kusaidia kukabiliana na tatizo la ukame au uhaba wa mvua.

Alisema polisi wamewekа utaratibu wa kupanda miti mara kwa mara na kwamba wataendelea kufanya hivyo kama sehemu ya utekelezaji wa majukumu yao.

Hivi karibuni Wakala Huduma za Misitu Tanzania TFS, Wilaya ya Mbeya ilitoa taarifa kwa umma kuwa wanayo miche ya kutosha kwa ajili ya kuzipatia taasisi na mashirika mbalimbali zinazohitaji kupanda miche ya aina mbalimbali kama vile ya miti na matunda.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa miche hiyo inatolewa bure, hivyo yeyote anayehitaji miche hiyo akifike kwenye ofisi cha TFS Wilaya ya Mbeya zilizopo eneo la Airport ya zamani kupatiwa miche hiyo.



# Wazazi na walezi watakiwa kuchunguza mienendo ya watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Jinsia wa Taasisi ya KFHI, Rosemary Mfui, amewataka wazazi na walezi kuchunguza mienendo ya watoto wao ili kuwakinga na vitendo vya udhalilishaji.

Alitoa rai hiyo jana wakati akitoa elimu ya jinsia na udhalilishaji wa kijinsia kwa wananchi wa Kigongoni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema baadhi ya wazazi na walezi huchangia kuwatengenezea mazingira mabovu watoto wao ikiwamo kuwatelekeza bila ya kuwapatia huduma muhimu za msingi. Hivyo aliwataka wazazi kushirikiana katika malezi ya watoto na kuwa na desturi ya kukaa na watoto wao ili kujua matatizo yanayowakabili.

Alisema pia watoto wanakabiliwa na matatizo mbalimbali hasa watoto wa kike, kwamba wanakumbana na vishawishi vingi hali inayosababisha kudhalilishwa na kushindwa kuendelea na masomo yao.

Alisema shirika lao linatekeleza mradi wa kuwahamasisha watoto wa kike kumaliza masomo yao kwa sababu kuna vikwazo vingi vinavyosababisha kutomaliza masomo yao ikiwamo ukatili wa kijinsia.

"Taasisi yetu inatekeleza mradi wa kutengeneza mazingira rafiki ya kujifunzia kwa wasichana kwa sababu kuna changamoto ya watoto kutembea umbali mrefu kwenda shule na uhaba wa vyoo shuleni,"alisema.

Meneja mradi wa taasisi hiyo, Yire Kim alisema kukosekana kwa ushauri nasaha kwa watoto wa kike kunasababisha kudhalilishwa na kushindwa kufikia malengo yao hasa ya kielimu.

Alisema sababu zingine ni mila na desturi potofu ambazo zinamkandamiza mtoto wa kike ikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Naibu wa Kiogoni, Malik Omar Hamad aliishukuru taasisi hiyo kwa elimu waliyoitoa kijijini hapo ambayo itasaidia katika mapambano ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.




Baadhi ya mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar akiwamo Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya (wa pili kushoto), wakikagua upakiaji wa makontena ya mizigo katika Bandari ya Malindi ya Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazanzibar wahimizwa kudumisha amani, utulivu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amesema bila ya uwapo wa amani na utulivu Zanzibar hakuna maendeleo yatakayopatikana.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga tamasha la amani yetu mshikamano wetu lililofanyika katika Uwanja wa Mao Zedong.

Mwita alisema Serikali ya Zanzibar ipo mstari wa mbele katika kuhimiza amani wakati wote, hivyo kuna kila sababu ya vijana waliyoshiriki tamasha hilo kuwa mabalozi wazuri wa jambo hilo.

Waziri huyo alisema imezoeleka ifikapo kipindi cha uchaguzi amani inakuwa tatizo, hivyo wakati umefika kwa vijana wa Zanzibar kuwa mstari wa mbele katika kuilinda amani wakati wote.

Aidha, aliwataka viongozi wa kisiasa kuwahimiza wafuasi wao kuwa mabalozi wazuri wa kuhimiza amani iliyopo kwa sababu chuki na vurugu hazisaidii maendeleo ya Zanzibar.

"Wakati huu wa kuiona Zanzibar katika kukuza uchumi wake ni lazima wananchi kuwa na uvumilivu ili kufikia maendeleo ya kweli ya serikali," alisema.

Balozi wa Ujerumani Tanzania, Regine Hess, alisema Tanzania ikiwamo Zanzibar ni mfano wa kuigwa katika kulinda amani hivyo kuna kila sababu ya vijana kuendelea kuitunza amani hiyo.

Alisema katika kufikia maendeleo ya taifa lolote lazima kuwe na amani ya kweli na watu wake na kwa baadhi ya nchi za Afrika baadhi yao zimekuwa zikingia katika migogoro katika vipindi vya uchaguzi.

Mratibu wa mradi huo, Amani Almas Ali, alisema kabla ya tamasha hilo wameshafanya makongamano kuhimiza amani kwa viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa ikiwamo na vijana.

Alisema makongamano hayo yalilenga kuwafanya vijana na viongozi wa kisiasa kuwa mabalozi wazuri, kuwaelimisha vijana wenzao juu ya kuhimiza amani iliyopo Zanzibar.

Alisema wanafahamu kuwa Zanzibar imekuwa na tatizo katika kipindi cha uchaguzi lakini kufanyika kwa mafunzo hayo itaonesha kuwa matatizo hayo yanaweza yasitokee tena.

Naye Mkurugenzi wa Mradi wa Kas Tanzania, Dk. Tilmann Feltes, alisema wameamua kushirikiana na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar kwa kuwashirikisha vijana ili ilete chachu ya maendeleo katika suala zima la kutatua migogoro hasa kudumisha amani na utulivu Zanzibar.

# Taasisi Bandari ya Malindi zahimizwa ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI za serikali zinazofanya kazi katika Bandari ya Malindi zimetakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa bidhaa wakati huu wa mfungo wa Ramadhani.

Mawaziri kutoka wizara tatu Zanzibar walieleza hayo jana wakati walipofanya ziara katika Bandari ya Malindi, eneo la kupatia mizigo la Bwawani pamoja na eneo la kuhifadhia kontena tupu liliopo Maruhubi.

Miongoni mwa mawaziri hao Waziri wa Fedha, Dk. Saada Mkuya, aliwataka wananchi wasiwe na wasiwasi wowote juu ya upatikanaji wa bidhaa za vyakula, kwamba serikali imejiridhisha chakula kipo cha kutosha.

Waziri wa Biashara na Maenedeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema lengo la ziara hiyo ni kujiridhisha juu ya upatikanaji wa bidhaa ya chakula hasa katika mwezi huu wa Ramadhan.

Pia, walipongeza jitihada zinazochukuliwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Shirika la Bandari kwa kuimarisha huduma za bandari jambo linalosaidia kukuza uchumi wa Zanzibar.

"Niwahakikishie wananchi kuwa hakuna ongezeko lolote la kodi katika bidhaa za chakula na serikali imefanya hivyo kwa makusudi kuwapa unafuu wananchi,"alisema.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alimshukuru Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa miongozo yake.

Alisema zaidi ya makontena 800 matupu yameondolewa katika eneo la bandari hadi sasa ili kutoa nafasi kwa makontena ya mizigo yanayoshushwa kutoka katika meli zinazokuja katika Bandari ya Malindi.

Waziri huyo alisema wizara yake kupitia Shirika la Bandari inachukua hatua ya kulifanya eneo la Maruhubi kutumika kama bandari kavu ya muda ili kuiongezea ufanisi Bandari ya Malindi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HASSANI ISSA SALUMU**
ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA TOWNACE NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI T418DHU, CHASSIS NO. SR500013548. ENGINE NO. 3SEAA3548. YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/104945/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WINGRED LEONARD NKOMA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI(NISSAN WAGON) YENYE NAMBA ZA USAJILI T 459 AJR MALI YA CARAVAN SAFARI LTD.
CHASIS NAMBA: VRGY60617699
ENGINE NAMBA: TD42057967
KADI NAMBA: 801316
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI RB NAMBA **IRI/IRI/RB/105569/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**BRIAN AMOS MBAGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4090-0172 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia NGARENARO SECONDARY SCHOOL mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/105295/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YADON MTARIMA KOHI**
ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAGARI AINA YA LAND CRUISER YENYE USAJILI NAMBA : T 754 AGN .KWA YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
POLISI TAARIFA: **KW/RB/1349/23**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Arumeru**
**Kituo cha KING'ORI**
**Mkoa ARUSHA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 03/2023**
**Jina la mdai JOSEPH KANDIDUSI LUOGA**
**Jina la Mdaiwa BERNEDICTA MARKI MROSSO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanunu ya 18 ya kanunu za Utaratibu Madai katika Mahakama za Mawnzo)**

**Kwa: BERNEDICTA MARKI MROSSO WA SHANGARAI**
Kwa kuwa Mdai/Mdaiwa ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (*eleza hapo habari za madai*) **FIKA MAHAKAMANI KUJIBU MADAI HAYA DHIDI YAKO**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 03 mwezi 04, Mwaka 2023 Saa 4:00 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hilini lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyousu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **23, Mwezi wa 03 Mawka 2023**


# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Kiongozi mkuu TPLF apewa nafasi Tigray

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, amemteua mwanachama mwandamizi wa chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF) Getachew Reda, kuwa mkuu wa utawala wa mpito katika jimbo la Tigray.

TPLF, ambayo ilipigana vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa miaka miwili dhidi ya serikali ya shirikisho, ilimteua Getachew wiki iliyopita kushika nafasi hiyo.

Katika vita hiyo, maelfu ya watu walikufa kwenye mapigano na kuibua mgogoro mkubwa wa kibinadamu. Pande zote zimeshutumiwa kutekeleza uhalifu wa kivita na utawala wa Marekani.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano ya amani ambayo TPLF na serikali ya muungano walitia saini nchini Afrika Kusini.

Utawala wa muda wa jimbo hilo, utakuwa madarakani hadi uchaguzi wa kikanda ufanyike chini ya usimamizi wa tume ya uchaguzi.

Baraza la wawakilishi la Ethiopia juzi liliiondoa TPLF katika orodha ya kundi la kigaidi. **BBC**

## Rais mteule aenda Ufaransa kupumzika

**ABUJA,** Nigeria

RAIS mteule wa Nigeria, Bola Tinubu, amefanya safari ya mapumziko katika nchi za Ufaransa na Uingereza.

Akiwa katika mapumziko hayo baada ya kushinda katika uchaguzi mkuu, Tinubu ataandaa mpango wa mpito kabla ya kuapishwa kwake Mei 29, mwaka huu.

Katika taarifa ya msemaji wa rais huyo mteule, Tunde Rahman, alisema kiongozi huyo mteule aliondoka nchini Jumanne.

Kulingana na Rahman, rais mteule baadaye atakwenda kufanya hija nchini Saudi Arabia.

"Rais mteule aliamua kupumzika baada ya kampeni na msimu wa uchaguzi wenye shughuli nyingi. Atapumzika Paris na London, katika kujiandaa kwenda Saudi Arabia kwa hija ndogo ya Umrah na mfungo wa Ramadhani," alisema Rahman.

Aliongeza kuwa Tinubu anatarajiwa kurejea nchini humo siku chache kabla ya kuapishwa kuwa rais.

Hata hivyo, safari za mara kwa mara za rais huyo mteule ng'ambo zinaendelea kuzusha uvumi kuhusu afya yake.

Alifanya safari kadhaa ambazo hazijatangazwa za kwenda Uingereza na Ufaransa kabla ya kuanza kwa kampeni mwaka jana.

Aidha, anakabiliwa na vita vya kisheria kuhusu ushindi wake katika uchaguzi wa rais wa mwezi uliopita. **BBC**

# Afrika Kusini kujadili hati kumkamata Rais Putin

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

**Waendesha mashitaka wa mahakama walisema huenda walihusika katika kuhamishwa kwa watoto wa Ukraine.**

AFRIKA Kusini imesema itashauriana na Russia kuhusu utekelezwaji wa hati ya kukamatwa kwa Rais wa nchi hiyo Vladmir Putin.

Shirika la habari la Russia (TASS) lilimnukuu Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, Naledi Pandor, kwamba mamlaka ya nchi hiyo itafanya mashauriano na Russia kuhusiana na hati ya kukamatwa kwa Putin, ambayo ilitolewa na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu ya Hague (ICC).

Mwezi Agosti mwaka huu, mkutano wa BRICS (Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini) utafanyika jijini Durban nchini humo na mamlaka zilisema ziliwaalika viongozi wa mataifa yote ya jumuiya hiyo, akiwemo Putin.

Wiki iliyopita, ICC ilitoa hati ya kukamatwa kwa Putin na mtoto wake Maria Lvova-Belova, akiwashuku kwa uhalifu wa kivita wakati wa uvamizi nchini Ukraine.

Waendesha mashitaka wa mahakama walisema huenda walihusika katika kuhamishwa kwa watoto wa Ukraine.

Tofauti na Russia, Afrika Kusini imeidhinisha Mkataba wa Roma, ambao unalazimika kuzingatia maamuzi ya Mahakama hiyo, ikiwa ni pamoja na kukamatwa kwa Putin.

Kwa mujibu wa TASS, Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini alisema kuwa suala la hati hiyo litajadiliwa na Russia.

"Tutasoma masharti ya sheria zetu, na, inaonekana, tutakuwa na majadiliano katika baraza la mawaziri , pamoja na wenzetu nchini Russia ili kuamua jinsi ya kuendelea," alisema Naledi Pandor, baada ya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje wa Sri Lanka ,Ali Sabri.

Awali msemaji wa Putin, Dmitry Peskov aliwaambia waandishi wa habari kwamba nchi yake bado haijatoa uamuzi kuhusu safari ya rais kwenda nchini Afrika Kusini. **BBC**



Wanawake wa Kiislamu wakihudhuria swala ya tarawih jioni ya kwanza ya mwezi mtukufu wa mfungo wa Ramadhani kwenye Msikiti wa Istiqlal huko jijini Jakarta, nchini Indonesia jana. **PICHA: REUTERS**



# Wakenya waonywa hatari kula nyama ya nguruwe

**NAIROBI,** Kenya

TAASISI ya utafiti wa magonjwa ya binadamu nchini Kenya (KEMRI), kwa ushirikiano na Shirika la Kulinda Wanyama Duniani, imewatahadharisha raia wa nchi hiyo kuhusu ulaji wa nyama ya nguruwe na kuku zinazouzwa katika maduka makubwa.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na watafiti hao, umebaini nyama inayouzwa kwenye maduka hayo ilikuwa na viwango vya bakteria wenye sugu kwa dawa, hivyo kuleta madhara kwa walaji.

Zaidi ya mwaka mmoja, sampuli zilikusanywa kutoka maduka mbalimbali makubwa katika miji mitano, ambayo ni Nairobi, Kisumu, Nakuru, Nanyuki na Eldoret, na kupelekwa katika maabara ya serikali.

Utafiti huo ulibaini kuwa bakteria hao wanaweza kuongezeka na kuwa janga kwa watu ambao wameathirika na ugonjwa huo.

Kulingana na Victor Yamo, mwanasayansi anayeshughulikia Ulinzi wa Wanyama Ulimwenguni, shida huanzia shambani wakati mkulima anawafuga nguruwe na kuku kwenye mazingira machafu.

Alisema ni muhimu kutekeleza viwango vya juu vya usafi wa chakula na usafi wa mazingira wakati wote wa ufugaji na usambazaji, haswa wakati wa kuchinja na ufugaji, ili kuzuia bakteria kuingia kwenye chakula.

Alilinganisha hali hiyo na janga ambalo linahatarisha maisha ya watu milioni tatu.

Yamo alisema ikiwa hali hiyo itaendelea, watu wasiopungua milioni 10 wanaweza kufariki dunia kila mwaka.

Mnamo 2019, mwandishi wa habari Dennis Okari, alifichua jinsi maofisa wa maduka hayo makubwa wasio waaminifu wanavyotumia kemikali kuongeza muda wa matumizi ya bidhaa za nyama. **BBC**

# SIMBA QUEENS YAPELEKA 'KILIO' CHAKE KWA MABEKI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya watani zao, Yanga Princess, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema safu yake ya ulinzi ilifanya makosa na kupelekea kugawana pointi katika mchezo huo wa dabi uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.

Matokeo hayo yaliiondoa Simba Queens kileleni katika msimamo wa ligi hiyo na kuwapisha Fountain Gate Princess iliyofikisha pointi 29 na kufuatiwa na JKT Queens yenye pointi 28.

Simba Queens yenye pointi 27, ambao ni mabingwa watetezi sasa wako katika nafasi ya tatu huku Yanga Princess yenye pointi 22 ikifuatia.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Lukula, alisema mchezo huo ulikuwa mzuri na walicheza vizuri kipindi cha kwanza na dakika 45 za mwisho walifanya makosa yaliyoruhusu wapinzani kupata bao la kusawazisha.**

Lukula alisema wachezaji wake hawakucheza vizuri kama alivyotarajia lakini anashukuru hawakupoteza mchezo huo na vita ya kutetea taji bado inaendelea.

"Hayakuwa matokeo mazuri kwetu kwa sababu malengo yetu ni kupata pointi tatu ambazo zingetufanya tuendelee kubaki juu katika msimamo, lakini tumeshindwa, tumefanya makosa yaliyotuadhibu, sasa tunarejea uwanja wa mazoezi kufanyia kazi madhaifu yetu.

Mapungufu mengine yalijitokeza katika mchezo huo ni sehemu ya viungo katika kipindi cha pili walipoteza mipira na sasa hilo halitajirudia katika mechi ijayo dhidi ya Fountain Gate," alisema Lukula.

Aliongeza wanahitaji kuendelea kupambana kutafuta matokeo mazuri ili kurejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Kocha Msaidizi wa Yanga Princess, Fred Mbuna, aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kupata alama moja mbele ya timu imara na nzuri.

Mbuna alisema haukuwa mchezo rahisi kwa pande zote mbili na mechi hiyo imepita wataendelea kujiimarisha kwa kufanyia kazi mapungufu yaliyopita ili mchezo unaofuata wapate ushindi.

"Mechi imeisha tumepata alama moja, tumecheza mpira mzuri kila mtu ameona, niwapongeze wachezaji wetu wamepambana kupata alama moja na sasa tunaenda kujipanga kwa ajili ya mechi ijayo," alisema Mbuna.



Wachezaji wa Yanga Princess pamoja na benchi la ufundi wakishangilia baada ya kupata bao la kusawazisha katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya mabingwa watetezi, Simba Queens, katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NBC yadhamini gofu Lugalo Open

**Na Shufaa Lyimo**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imekabidhi Sh. milioni 10 kwa ajili ya kudhamini mashindano ya gofu ya Lugalo Open yatakayofanyika Machi 25 na 26, mwaka huu, Dar es Salaam.

Mwakilishi wa benki hiyo, Elibariki Masuke, alisema anaipongeza klabu ya Lugalo kwa kuwashirikisha katika mashindano mbalimbali ya mchezo huo.

"Tunathamini michezo, pia tunatambua inaleta maendeleo pamoja na kuongeza kipato cha nchi yetu na kwa lengo la kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tunaamini udhamini huu utaongeza hamasa katika mchezo wa gofu," alisema Masuke.

Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo, Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana, watu wazima, wachezaji wa ridhaa na wachezaji wa kulipwa.

Luwongo alisema Waziri wa Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ndiye atakuwa mgeni rasmi atakayefungua mashindano hayo.

Enock Magile, mwakilishi wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Gilman Kasiga, alisema wamefurahi kupata udhamini huo ambao utawaongezea morali wachezaji wao.

"Tunapata faraja kuona tunazidi kufanya kazi pamoja na wenzetu wa NBC, hatutaishia hapa, bado kuna mashindano mengi ambayo yanaendelea katika klabu hii," alisema Magile.

## SBL yawafunda wasanii wanawake

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kushirikiana na Mdundo, wameendesha semina ya uwezeshaji wasanii wa muziki wa kike hapa nchini ili kuwapa ujuzi utakaowasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali katika tasnia hiyo dhidi ya wanaume.

Semina hiyo imefanyika baada ya Mdundo kufanya utafiti na kubaini wasanii wa kike wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo rushwa ya ngono.

"Hii ni fursa kwetu kuunga mkono sauti za kimaendeleo na kupigania ushirikishwaji kulingana na malengo yetu ya 'Society 2030, kutoa msaada kwa wasanii wa kike kunaimarisha zaidi msimamo wetu wa kusimamia tofauti za kijinsia," Meneja Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu, alisema.

Meneja wa Leseni na Ushirikiano wa Mdundo, Prisna Nicholaus, alisema baada ya kubaini changamoto hizo, hatua iliyofuata ilikuwa ni kutengeneza jukwaa litakalowaweka pamoja wasanii hao na kujifunza kukabiliana na matatizo hayo kutoka kwa wenzao wenye uzoefu.

Jumla ya wanajopo 10 wakiwamo wawakilishi kutoka COSOTA, vyombo vya habari, makampuni ya usambazaji wa muziki na leseni pamoja na SBL walitoa mafunzo katika semina hiyo.

## KMC yasaka pointi Ligi Kuu vidoleni

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya KMC ambayo ipo katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 26, imeingia kambini kuanza maandalizi ya mechi zilizosalia huku ikisema inahakikisha inafanya vyema na kusalia katika ligi hiyo.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, aliliambia gazeti hili kimahesabu mpaka sasa ukiondoa Simba, Yanga, Singida Big Stars na Azam FC, timu zote zinaweza kushuka daraja au kucheza mechi za mchujo.



Mwagala alisema wana uhakika wa kufanya vizuri katika mechi tano zilizosalia ambazo mbili watacheza nyumbani na kujiondoa kwenye hatari.

Alizitaja mechi zao zilizobakia ni dhidi ya Geita Gold, Singida Big Stars, Dodoma Jiji, Prisons na Mbeya City.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kwa muda kupisha mechi za kimataifa ambapo leo Taifa Stars itakuwa ugenini dhidi ya Uganda na itarudiana nao Machi 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### GNONTO AGOMBEWA EPL

ARSENAL, Chelsea na Manchester City zimeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Italia, Wilfried Gnonto, 19, ambaye anaichezea Leeds United. ***(Gazzetta dello Sport, Via Metro)***

### JUVENTUS, NAPOLI ZAJITOSA

JUVENTUS na Napoli ni miongoni mwa klabu kadhaa za Italia ambazo vinavutiwa na huduma ya mshambuliaji wa Italia, Wilfried Gnonto, 19. ***(90min)***

### YAMKOMALIA HENDERSON

KLABU ya Manchester United inaweza kutumia nia ya Tottenham Hotspur kumnunua mlinda mlango, Dean Henderson, 26, kama kishawishi cha Spurs kumuuza mshambuliaji wake, Harry Kane (29). ***(ESPN)***

### MUANI ANUKIA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Eintracht Frankfurt na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Randal Kolo Muani, 24, ambaye analengwa kwa pauni milioni 105 na Manchester United, amependekeza yuko tayari kuhama msimu huu. ***(L'Equipe, Via Mail)***

### WIRTZ ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imefufua nia yao ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Florian Wirtz, 19. ***(90min)***

### POCHETTINO AKARIBIA MADRID

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye hatari ya kumkosa kocha wake wa zamani, Mauricio Pochettino, katika msimu wa joto huku raia huyo wa Argentina akiwa kwenye orodha ya juu ya walimu wanaowaniwa na Real Madrid iwapo kocha wa sasa Carlo Ancelotti ataondoka. ***(Times)***

### LUKAKU KUIUMIZA CHELSEA

CHELSEA imekubali itahitaji kupata hasara kubwa ikiwa inataka kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, 29, ifikapo msimu wa joto. ***(Football Insider)***

### ZUBIMENDI AIKATAA BARCA

MATUMAINI ya Arsenal na Barcelona kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi, 24, kutoka Real Sociedad yanaonekana kuisha baada ya mchezaji huyo kusema hatarajii kuondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

### VANDERSON KUTUA BARCA

BARCELONA imeonyesha nia ya kumsajili beki wa Monaco, Vanderson, 21. ***(Sport)***

### WILLIAMS AINGIA SOKONI

KLABU kadhaa zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa kushoto, Brandon Williams, 22, kutoka Manchester United. ***(Football Insider)***

### RABIOT AITAKA LIVERPOOL

KIUNGO wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot, 27, amedokeza huenda akavutiwa na uhamisho wa kuelekea Liverpool. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# RONALDO ATABIRI UKUBWA LIGI YA SAUDIA ARABIA

**Nyota huyo asema itakuwa bora duniani endapo wataendelea kuwekeza...**

**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo ana imani Ligi Kuu ya Saudi Arabia (Saudia Pro League) itakuwa mojawapo ya mashindano bora zaidi duniani katika miaka ijayo.

**Nahodha huyo wa Ureno alijiunga na Al Nassr ya Saudi Arabia baada ya fainali za Kombe la Dunia mwaka jana, akimaliza kipindi chake cha pili akiwa na Manchester United ambacho kiliisha ghafla kabla ya michuano hiyo iliyofanyika Qatar.**

Akiwa mchezaji huru baada ya Ureno kutolewa katika robo fainali mikononi mwa Morocco, Ronaldo alihamia Mashariki ya Kati mara moja na ametulia kwa haraka, akifunga mabao tisa katika mechi nane za ligi hiyo.

Ingawa inachukuliwa ligi dhaifu kuliko zile za Ulaya, Ronaldo anaamini mechi hizo zimetayarisha kwa majukumu ya Ureno na anatarajia sifa ya Ligi Kuu ya Saudia kuimarika kwa wakati.

"Ninajisikia vizuri," alisema kabla ya Ureno kucheza mechi kufuzu Euro 2024 dhidi ya Liechtenstein. "Ndio maana niko hapa. Kama sikuwaza hivyo, nisingekuwa.

"Niko kwenye ligi yenye ushindani mkubwa, wanapaswa kuangalia michuano ya Saudia kwa njia tofauti.

"Ni wazi si kama Ligi Kuu England, ningesema uongo, lakini ina ushindani, nashangazwa na nguvu, ina timu nzuri, ina uwiano, wachezaji wa Kiarabu ni wazuri.

"Inawezekana, katika muda wa miaka mitano hadi sita, ikiwa wataendelea na mpango huu, itakuwa ligi yenye ushindani mkubwa duniani."

Kurejea kwa Ronaldo, United hakukuisha kama alivyotarajia na alitafakari kipindi kigumu.

Alisema: "Wakati mwingine lazima upitie mambo machache ili kuona nani yuko upande wangu. Katika hatua ngumu, unaona nani yuko upande wako.

"Sina shida kusema nimekuwa na wakati mbaya katika maisha yangu, lakini hakuna wakati wa majuto."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,093,3

MECHI KALI
UGANDA
VERSUS
TANZANIA
1 | 2.31
X | 3.09
2 | 3.19

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SOUTHGATE: KANE SASA YUKO SAWA



**LONDON,** England

HARRY Kane amesahau yote baada ya matokeo mabaya katika Kombe la Dunia lililopita, amesema Kocha wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate.

Nahodha huyo wa Simba Watatu alikosa penalti katika mchezo wa robo fainali dhidi ya Ufaransa nchini Qatar, hivyo kuendeleza taifa hilo kusubiri kwa muda mrefu kutwaa taji hilo.

Kane angevunja rekodi ya kimataifa ya Wayne Rooney kama angefunga penalti na vilevile angeweza kuiongoza England kutinga nusu fainali, lakini akapiga shuti kali juu ya goli na wakapoteza kwa kufungwa mabao 2-1.

Hayuko peke yake katika maumivu ya moyo ya penalti kwa England, wachezaji wenzake Bukayo Saka, Marcus Rashford na Jadon Sancho wote wakikosa penalti katika mechi ya kichapo cha penalti dhidi ya Italia kwenye uwanja wa Wembley katika fainali ya Euro 2020.

Tukirudi nyuma zaidi, Southgate mwenyewe alikosa nafasi katika ushindi wa England katika nusu fainali ya Ujerumani kwenye michuano ya Euro 1996, kumaanisha Kane ndiye nyota wa hivi karibuni zaidi katika msururu wa nyota kupata maumivu ya moyo ya penalti.

Hata hivyo, Southgate anahisi hilo halitamrudisha nyuma mshambuliaji huyo wa Tottenham na kumuunga mkono kama mmoja wa magwiji wa muda wote.

"Tumeona hilo kwa uchezaji wake na malengo yake kwa klabu yake," alisema.

Heshima ya kuwa mfungaji bora wa mabao wa England inakaribia kumwangukia Kane, ambaye anafungana na Rooney mwenye mabao 53.



# Mesut Ozil atangaza kustaafu

**LONDON,** England

KIUNGO wa zamani wa Arsenal na Real Madrid, Mesut Ozil, ametangaza kustaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 34.

Ozil, ambaye alikuwa katika kikosi cha Ujerumani kilichoshinda Kombe la Dunia mwaka 2014, ametumia misimu mitatu iliyopita kwenye Ligi Kuu Uturuki na amestaafu baada ya kucheza mechi nne za ligi akiwa na Basaksehir, ambayo alijiunga nayo akiwa mchezaji huru mwaka jana.

Mwaka 2018 alistaafu kuichezea Ujerumani huku kukiwa na mjadala wa kisiasa nchini humo kuhusu kufurika kwa wahamiaji na baada ya kukashifiwa kuhusu picha iliyopigwa na Rais wa Uturuki, Tayyip Erdogan, akisema alikabiliwa na "ubaguzi wa rangi na kutoheshimiwa" juu ya asili yake ya Kituruki.

Kiungo huyo alicheza mechi 645 katika klabu za taifa, zikiwamo 254 akiwa na Arsenal katika kipindi cha miaka saba.

Alishiriki katika fainali za Kombe la FA mwa 2014, 2015 na 2017, na k saidia timu yake kushin katika mechi zote tatu Wembley.

"Baada ya kutafaka kwa kina, ninatanga kustaafu mara moja k toka kwenye soka ya k lipwa," alindika Ozil kati kwenye ukurasa wake w Twitter.

"Nimekuwa na fursa kuwa mchezaji wa kulipw kwa takriban miaka 17 sa na ninahisi kushuku sana kwa nafasi hiyo," O alisema.

395,265/-

# LIGI KUU ZANZIBAR KUENDELEA MEI 6

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu Zanzibar imesimama kupisha mwezi mtukufu wa Ramadhani na inatarajiwa kuendelea tena kuanzia Mei 6, mwaka huu, imefahamika.

Ligi hiyo imesimama ikiwa timu zote zimecheza michezo 25 na kubakisha michezo mitano ili kumaliza msimu na kupata bingwa atakayeiwakilisha Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Licha ya kubakisha michezo michache lakini hakuna timu ambayo imeukaribia Ubingwa kutokana na timu zinazoutaka Ubingwa huo KMKM na KVZ kupishana alama moja.

**KMKM ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 54 wakifuatiwa na KVZ yenye alama 53 na nafasi ya tatu inashikiliwa na Mlandege yenye pointi 47.**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, alisema jana ligi hiyo imesimama ikiwa ni utaratibu ambao umezoeleka Zanzibar kila Ramadhani inapoingia.

"Tumekuwa na utamaduni wa ligi yetu kusimama kuupisha mwezi huu mtukufu, tunatoa nafasi kwa wachezaji na viongozi kushiriki ibada hii kikamilifu," alisema Salum.

Aliongeza bado hakuna timu yenye uhakika wa kutwaa taji hilo kwa sababu lolote linaweza kutokea katika mechi tano zilizobakia.

Hata hivyo tayari Bodi ya Ligi imeshatoa ratiba ya michezo iliyobaki ambayo itachezwa kwenye viwanja vya Amaan na Finya vilivyoko Kisiwani Pemba.



Wachezaji wa timu ya wenye ulemavu ya Sauti Parasports FC wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenzao kutoka Kenya itakayochezwa hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## MobiAd yaipatia Simba

INATOKA UKURASA 24

"Ni safari ndefu ambayo inahitaji mshikamano, tumeamua kufanya kazi na Simba, ni timu kubwa barani Afrika ambayo iko mstari wa mbele katika kukuza soka la vijana," alisema Sikoni.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah "Try Again' naye aliishukuru kampuni hiyo na kuongeza mazungumzo ya kufanikisha udhamini huo hayakuwa rahisi.

"Hakuna miujiza kwenye soka ili kupata timu nzuri unapaswa kuwekeza kwa vijana, tunaamini pesa hizi zitatimiza malengo yenu na yetu, Simba ina malengo ya kuchochea soka la vijana," alisema Try Again.

## Stars matumaini

INATOKA UKURASA 24

vizuri katika michuano ya kimataifa huku Taifa Stars inafanya vizuri na kufuzu kucheza fainali ya AFCON mwakani.

Anaimani na timu ya Tanzania itafanya vizuri katika mchezo wa kesho (leo), kupambana kutafuta pointi tatu muhimu na kurejea nyumbani, siku ya Jumanne nyumbani kuvuna alama nyingine," alisema Majaliwa.

Kupitia Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah, klabu hiyo imetoa tiketi 1,000, Mwenyekiti, Murtaza Mangungu naye ametoa tiketi 100, Yanga tiketi 1,500 na Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' amesema wao watatoa tiketi 1,000.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Lameck Nyambaya, alisema anatoa tiketi 200.

Mchakato huo wa kuhamasisha kutoa tiketi uliongozwa na Maofisa Habari kutoka Simba, Yanga na Azam FC.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/03/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Northampton Town | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 02. 25/03/23 | 18:00 | Peterborough United vs Derby County | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 03. 25/03/23 | 18:15 | Racing Santander vs Levante UD | 3.45 | 3.00 | 2.15 |
| 04. 25/03/23 | 18:15 | UD Ibiza vs Burgos CF | 2.33 | 2.80 | 3.30 |
| 05. 25/03/23 | 23:00 | Bogota FC vs Tigres FC | 2.27 | 2.85 | 2.90 |
| 06. 25/03/23 | 23:30 | Portland Timbers vs Los Angeles Galaxy | 2.14 | 3.30 | 2.70 |
| 07. 26/03/23 | 02:30 | DC United vs New England Revolution | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 08. 26/03/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 2.39 | 3.00 | 2.60 |
| 09. 26/03/23 | 02:30 | Columbus Crew vs Atlanta United FC | 2.40 | 3.10 | 2.50 |
| 10. 26/03/23 | 03:30 | Houston Dynamo vs New York City FC | 2.44 | 3.10 | 2.45 |
| 11. 26/03/23 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Seattle Sounders | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 12. 26/03/23 | 04:05 | CF Correcaminos UAT vs CD Mineros de Zacatecas | 2.16 | 2.95 | 2.95 |
| 13. 26/03/23 | 06:05 | Pumas de Tabasco vs Raya2 Expansion | 2.49 | 2.95 | 2.49 |
| 14. 26/03/23 | 08:00 | Iwaki FC vs Machida Zelvia | 2.50 | 2.95 | 2.47 |
| 15. 26/03/23 | 15:30 | FC Dordrecht vs Helmond Sport | 2.47 | 3.15 | 2.39 |
| 16. 26/03/23 | 17:15 | SD Ponferradina vs CD Mirandes | 2.07 | 3.10 | 3.50 |
| 17. 26/03/23 | 17:15 | Real Zaragoza vs Albacete Balompie | 2.10 | 3.00 | 3.50 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 24/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3863 | Japan vs Uruguay | 2.46 | 3.23 | 2.90 |
| 14:00 | 1948 | South Korea vs Colombia | 2.85 | 3.12 | 2.58 |
| 16:00 | 2250 | DR Congo vs Mauritania | 1.51 | 3.83 | 6.81 |
| 16:30 | 2141 | Ukraine U21 vs Denmark U21 | 3.42 | 3.31 | 1.98 |
| 17:00 | 4134 | Uganda vs Tanzania | 2.31 | 3.09 | 3.19 |
| 19:00 | 1777 | Nigeria vs Guinea Bissau | 1.38 | 4.47 | 8.09 |
| 19:00 | 3205 | South Africa vs Liberia | 1.36 | 4.56 | 8.70 |
| 19:00 | 3359 | Ivory Coast vs Comoros | 1.26 | 5.20 | 11.67 |
| 19:00 | 4048 | Cape Verde vs Eswatini | 1.35 | 4.47 | 9.37 |
| 20:00 | 1012 | Czech Republic U21 vs Belgium U21 | 2.96 | 3.17 | 2.24 |
| 20:00 | 3322 | Samsunspor vs Altinordu | 1.34 | 4.51 | 6.97 |
| 20:00 | 4702 | Bulgaria vs Montenegro | 2.59 | 3.16 | 2.88 |
| 20:00 | 5456 | Romania U21 vs Portugal U21 | 4.67 | 3.58 | 1.65 |
| 20:00 | 5692 | Denizlispor vs Boluspor | 3.03 | 3.24 | 2.12 |
| 20:30 | 1501 | Sedan vs Dunkerque | 2.46 | 3.14 | 2.78 |
| 20:30 | 1635 | Red Star vs Orleans | 1.86 | 3.41 | 3.94 |
| 20:30 | 1913 | Villefranche Sur Saone vs Concarneau | 3.10 | 3.15 | 2.25 |
| 20:30 | 2773 | Avranches vs Le Puy | 2.21 | 3.16 | 3.16 |
| 20:30 | 3247 | Paris 13 Atletico vs Bourg Peronnas | 2.63 | 3.01 | 2.69 |
| 20:30 | 5021 | Cholet vs FC Versailles 78 | 2.84 | 3.11 | 2.43 |
| 20:30 | 5253 | Chateauroux vs Bastia Borgo | 1.40 | 4.42 | 6.94 |
| 21:00 | 2340 | Uzbekistan vs Bolivia | 2.39 | 3.23 | 3.01 |
| 22:00 | 2531 | Anguilla vs Saint Lucia | 6.65 | 4.78 | 1.35 |
| 22:00 | 3032 | Saudi Arabia vs Venezuela | 2.33 | 3.23 | 3.12 |
| 22:00 | 3839 | Senegal vs Mozambique | 1.32 | 4.78 | 9.78 |
| 22:00 | 4392 | Mali vs Gambia | 1.55 | 3.88 | 5.95 |
| 22:00 | 5652 | Equatorial Guinea vs Botswana | 1.63 | 3.46 | 5.97 |
| 22:00 | 5957 | Egypt vs Malawi | 1.34 | 4.48 | 9.81 |
| 22:30 | 4854 | Clyde vs Airdrieonians | 4.67 | 3.79 | 1.62 |
| 22:45 | 1194 | Dungannon Swifts vs Linfield Belfast | 11.28 | 5.33 | 1.20 |
| 22:45 | 1216 | France vs Netherlands | 1.93 | 3.53 | 4.02 |
| 22:45 | 1765 | Bray Wanderers vs Wexford Youths | 2.03 | 3.32 | 3.17 |
| 22:45 | 2179 | Kerry FC vs Athlone Town | 3.38 | 3.48 | 1.90 |
| 22:45 | 2181 | Gap Connahs Quay vs Newtown AFC | 1.58 | 3.82 | 4.86 |
| 22:45 | 2649 | Ayr United vs Cove Rangers | 1.59 | 3.90 | 4.78 |
| 22:45 | 2814 | Gibraltar vs Greece | 22.86 | 7.62 | 1.14 |
| 22:45 | 2852 | Falkirk FC vs Kelty Hearts FC | 1.53 | 4.06 | 5.10 |
| 22:45 | 2881 | Sweden vs Belgium | 3.21 | 3.37 | 2.26 |
| 22:45 | 3083 | Edinburgh City vs Queen of South | 2.97 | 3.33 | 2.19 |
| 22:45 | 3286 | Queens Park vs Arbroath | 1.80 | 3.49 | 3.96 |
| 22:45 | 3574 | Czech Republic vs Poland | 2.45 | 3.26 | 2.98 |
| 22:45 | 4035 | Austria vs Azerbaijan | 1.29 | 5.46 | 10.93 |
| 22:45 | 4539 | Galway United vs Longford Town | 1.31 | 4.53 | 8.03 |
| 22:45 | 5032 | Moldova vs Faroe Islands | 2.58 | 3.10 | 2.94 |
| 22:45 | 5702 | Serbia vs Lithuania | 1.15 | 7.37 | 22.76 |
| 23:00 | 1630 | Bahamas vs Trinidad and Tobago | 11.38 | 5.59 | 1.20 |
| 23:00 | 2063 | Spain U21 vs Switzerland U21 | 1.53 | 3.84 | 5.40 |
| 23:00 | 3818 | Burkina Faso vs Togo | 1.68 | 3.50 | 5.31 |
| 23:30 | 4314 | Tunisia vs Libya | 1.33 | 4.59 | 9.81 |
| 23:30 | 5096 | Cameroon vs Namibia | 1.40 | 4.27 | 8.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo


Ijumaa Machi 24, 2023

Nipashe




Ozil atangaza kustaafu

UKURASA 22




Kaimu Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya MobiAd Africa, Lumisho Sikoni (kulia), akiwakabidhi hundi ya mfano ya Sh. milioni 500 viongozi wa Simba, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim Abdallah 'Try Again' (kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi, Imani Kajula, baada ya kusaini mkataba wa kuendeleza soka la vijana katika klabu hiyo. **PICHA: SAADA AKIDA**

# STARS MATUMAINI IKIWAVAA UGANDA

## ●●● Rais Samia aongoza kununua tiketi za mashabiki kuishangilia timu hiyo katika...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

TIMU zote zikiwa ugenini, kikosi cha soka cha Tanzania (Taifa Stars), kinatarajia kuikabili Uganda (Cranes) katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Afrika (AFCON), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Suez Canal ulioko Ismailia, Misri.

**Fainali zijazo za AFCON zitafanyika Ivory Coast baadaye mwaka huu na Uganda imechagua kutumia uwanja huo kutokana na viwanja vya nyumbani kwao kutokidhi vigezo viliyowekwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).**

Itakuwa ni mechi muhimu kwa pande zote mbili kwani zina pointi moja kwenye Kundi F, hivyo mshindi yoyote hapo atakuwa amefufua matumaini ya kusonga mbele.

Kocha Mkuu wa Stars, Adel Amrouche, amesema wachezaji wake wana morali na wapo tayari kwa ajili ya mechi hiyo.

"Tuna wachezaji wazoefu na vijana. Siangalii mapungufu yaliyopo, naangalia kile kizuri ambacho tunacho na tutakwenda kukifanya, huwezi kusema huna muda wa kutosha kwa sababu hata wenzetu nao pia hawakuwa na muda," alisema Amrouche.

Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta, alisema haijawahi kutokea mechi kati ya Tanzania na Uganda ikawa rahisi, hivyo anatarajia itakuwa ngumu, lakini wachezaji wote wamejipanga kufanya kila linalowezekana ili kuibuka na ushindi.

"Watanzania mpinzani wetu mgumu zaidi Afrika Mashariki kucheza nao ni Uganda, nakumbuka kuna mechi hivi karibuni tuliwafunga na hii tutahakikisha tunashinda," alisema Samatta.

Stars ilianza michuano hiyo Juni 4, mwaka jana ilipolazimisha sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Niger, lakini nyumbani ikachapwa mabao 2-0 dhidi ya Algeria, mechi iliyochezwa siku nne baadaye.

Mechi nyingine ya kundi lao itakuwa ni kati ya Algeria dhidi ya Niger, waarabu hao wenye pointi sita ndio wanaoongoza wakati wageni wao wana pointi mbili kibindoni.

Wakati huo huo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, atatoa tiketi 4,000 kwa mashabiki watakaojitokeza kushuhudia mchezo wa marudiano kati ya Stars dhidi ya Uganda utakaochezwa Jumanne.

Jumla ya tiketi 10,500 zimepatikana ambazo zitagawiwa kwa mashabiki zilizotolewa na viongozi na wadau mbalimbali wa soka nchini zikiwamo klabu za Simba, Yanga na Azam FC kwa lengo la kuhamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani.

Ofisa wa Habari na Mawasiliano ya Shirikisho la Soka Afrika (TFF), Clifford Ndimbo, amefanya hamasa kwa kukusanya tiketi kutoka kwa wadau wa soka nchini ili kufanikisha mashabiki kuingia kwa wingi katika mchezo huo wa marudiano.

Kupitia simu ya Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema Rais Samia ametoa tiketi 2,000 kwa mashabiki na yeye ametoa 1,000.

"Juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha Tanzania inaendelea kufanya

INAENDELEA UKURASA 23

# MobiAd yaipatia Simba mamilioni

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaendeleza soka la vijana, Uongozi wa Simba na Kampuni ya MobiAd Africa wameingia mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya Sh. milioni 500, imeelezwa jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla maalumu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula, alisema anawashukuru MobiAd Africa kwa udhamini huo kwa sababu kanuni ya mafanikio siku zote lazima iwe na mwanzo.

"Simba inakwenda mbele kutambua vipaji na kuvichukua, kuviendeleza na kutengeneza timu yenye vipaji vikubwa sana, tunaamini Simba imara yenye vipaji haitaisaidia Simba pekee bali hata taifa letu," alisema Kajula.

Aliongeza kanuni ya mafanikio ya kila kitu lazima kianzie mwanzo, Simba wameona umuhimu wake wamerudi kwenye njia zao za zamani na kutamba wanaongoza kutoa wanaocheza kwa mkopo katika timu nyingine za Ligi Kuu Bara na za daraja la kwanza.

"Ni safari ndefu ambayo inahitaji mshikamano tuna mategemeo chanya huu ni mwanzo tu kuna udhamini mkubwa unakuja tumeamua kufanya kazi na Simba ni timu kubwa barani Afrika ambayo iko mstari wa mbele katika kukuza soka la vijana.

Tunataka kuondoa bahati kwenye mpira na tunataka kuwaandaa vijana wenye vipaji ili baadaye kuja kuisaidia timu na vijana watakaopatikana tutawasomesha Simba wenyewe," alisema Kajula.

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu wa MobiAd Africa, Lumisho Sikoni, alisema anaishukuru Simba kwa kuwapa nafasi ya kufanya nao kazi kwa sababu wanafahamu vijana ni taifa la kesho hivyo matayarisho yao yanapaswa kuanza leo.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >